Mwongozo Wa Mwanafunzi

8

# Utiifu kwa Mungu

## Kujifunza Kunyenyekea kwa Mwongozo wa Mungu



MVMM
Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

# Utiifu kwa Mungu

## Kujifunza Kunyenyekea kwa Mwongozo wa Mungu

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwanafunzi

Toleo la Tano

MVMM
Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

# Utiifu kwa Mungu

## Kujifunza Kunyenyekea kwa Mwongozo wa Mungu

Kimeandikwa Na David Batty
Mwongozo Wa Mwanafunzi
Toleo la tano

Maandiko yanayotumiwa katika kitabu hiki yametoka kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2024, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii yaKiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwenye mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo: *Obedience to God, 5th edition.*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, mashuleni, katika huduma gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vile vile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, kitabu cha kuongoza mafunzo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.org na
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 01-2024

# Yaliyomo

**Sura ya 1. Upendo na Utiifu....4**
- A. Hitaji la Mahusiano mapya....4
- B. Je, utii una nafasi gani katika uhusiano wangu na Mungu? ....7
- C. Kwa nini umtii Mungu? ....8
- D. Ninawezaje kutii sheria kuu ya Mungu? ....9
- E. Je, nia za mtu huwa na nafasi gani katika kumtii Mungu?....11

**Sura ya 2. Mitazamo na Utiifu....14**
- A. Angalia mitazamo inayofanya iwe rahisi kutomtii Mungu ....14
- B. Kuza mitazamo ya utiifu ....15
  1. Tabia ya heshima....16
  2. Mtazamo wa mtumishi ....17
  3. Mtazamo wa shukrani (nia ya shukrani) ....17
  4. Mtazamo wa utulivu....18

**Sura ya 3. Ni sheria zipi nina paswa kutii? ....20**
- A. Aina za sheria za Mungu....21
- B. Mjadala kuhusu nisheria zipi tunapswa kutii leo ....22
- C. Tii kanuni zinazoshikilia sheria za Mungu....24
- D. "Mapenzi ya Mungu" ni nini? ....26

**Sura ya 4. Matokeo ya kumtii Mungu ....29**

**Sura ya 5. Matokeo ya kutomtii Mungu....33**
- A. Ninaweza kujifunza nini kutokana na kutotii kwa wengine?....33
- B. Maneno manne muhimu yanayohusiana na kutotii....35
- C. Je, Mtazamo wa Mungu ni nini kwa watu wasiotii sheria zake? ....39

# Sura ya 1
# Upendo na Utiifu

Labda unakumbuka siku uliyokubali kuwa Mkristo. Ikiwa hilo lilitokea katika miezi michache iliyopita, basi unaweza kukumbuka kwa urahisi jinsi maisha yako yalivyokuwa kabla uwe Mkristo.

Uzoefu wa kuwa Mkristo ni zaidi ya kuomba tu maombi rahisi-yote ni kuhusu kuingia kwa uhusiano mpya na Mungu. Tunaondokea kuwa maadui wa Mungu na kuwa rafiki maalum wa Mungu.

**Wakolosai 1:21-22 Biblia Takatifu (SUV)**

**Hii ni pamoja na wewe ambaye wakati mmoja ulikuwa mbali sana na Mungu. Mlikuwa maadui zake, mkiwa mmejitenga naye kwa mawazo yenu mabaya na matendo yenu, [22] lakini sasa amewarudisha ninyi kuwa marafiki wake. Amefanya hivi kupitia kifo chake msalabani katika mwili wake mwenyewe wa kibinadamu. Kama matokeo, amekuleta mbele za Mungu, na wewe ni mtakatifu na huna lawama unaposimama mbele zake bila kosa hata moja.**

Mungu anataka tuelewe ni kwa kiasi gani anatupenda. Anataka kutuchukua kama watoto Wake.

**Wagalatia 3:26 Biblia Takatifu**

**Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu.**

Unapojifunza kozi hii, chukua wa muda kujiuliza maswali haya kwa uangalifu.

Inamaanisha nini kuwa mwana au binti wa Mungu?

Je, tunakuzaje uhusiano wetu na mtu ambaye hatuwezi kumuona?

Je, nina uhusiano wa aina gani na Mungu?

## A. Hitaji la Mahusiano mapya

### 1. Je, ni mahusiano gani unayothamini zaidi leo?

Mungu anataka tuone kuwa kuwa Mkristo ni zaidi ya tikiti ya kuingia mbinguni tu. Mungu anataka tuwe na uhusiano wa kibinafsi naye leo. Tunapokuwa Wakristo, Mungu anataka tuangalie kwa makini mahusiano tuliyo nayo maishani mwetu na tuanze kuyabadilisha inapohitajika.

Utamaduni wetu unathamini sana uhuru. Jumbe za kitamaduni ni pamoja na: “Usiruhusu mtu yeyote akutawale.” “Simamia maisha yako mwenyewe.” “Ikiwa wewe ni kijana, lazima upiganie uhuru wako.”

Lakini Mungu anataka tuthamini uhusiano wetu naye zaidi ya kila uhusiano mwingine wowote. Na Yeye anataka uhusiano huo ukue na kukomaa. Ikiwa ulikuwa na kaka au dada mchanga, au mtoto wako mwenyewe, umeona jinsi alivyokuwa na uhusiano na mtoto. Mtoto huyo anapokua, uhusiano wako unabadilika-tunatumai! Ikiwa bado wanafanya mambo kama mtoto wa miaka 2 wakati wana miaka 20, si vyema tena- hii ni shida sasa.

Vivyo hivyo Mungu anataka tukue na kukuza uhusiano wetu naye ambao unabadilika - unakomaa. Anataka uwe mwanachama mkomavu wa familia Yake.

## 2. Je, tunakuzaje mahusiano mapya?

Unapokuwa Mkristo unahitaji kuangalia kwa uangalifu watu ulio karibu sana nao kama marafiki zako. Je, Marafiki hawa wanakusaidia kumjua Mungu vyema? Au wanakurudisha nyuma kwenye maisha yako ya zamani ya dhambi uliyokuwa ukiishi kabla ya kuwa Mkristo?

Mungu anataka uwe na marafiki ambao watakusaidia kukua ile uwe kila kitu alichokuumba uwe. Itabidi usitishe baadhi ya mahusiano ambayo yatazuia uhusiano wako na Mungu. Lakini hata ukuwa na marafiki Wakikristo, unahitaji kujiuliza, “Je, Rafiki huyu ananisaidia kukua nikiwa karibu na Mungu?”

Kwa hivyo unakuzaje uhusiano wa kina zaidi na Mungu? Njia ya kukomaa ni ipi? Hapa kuna orodha ya maeneo kadhaa muhimu ya maisha yako ambayo yatakusaidia kukua na kuwa mtu aliyekomaa ambaye Mungu anataka uwe.

- Upendo
- utiifu - Yohana 14:15
- Kuifanya upya akili yako - Warumi 12:1-2
- Jifunze jinsi ya kupinga majaribu ya kutenda dhambi - Yakobo 4:7-8
- Tembea kwa uaminifu katika uhusiano wako na Mungu na wengine
- Jifunze jinsi ya kuwa mtu wa kweli
- Jifunze jinsi ya kufurahia maisha
- Jifunze jinsi ya kuishi kwa uhuru - uhuru wa kweli, bila kuwa katika kifungo cha dawa za kulevya, chakula, pesa, mahusiano, au kitu kingine chochote.

## 3. Mungu anataka kuwa baba yako

Unapokuwa Mkristo, inamaanisha kwamba umemuomba Mungu awe Kiongozi wa maisha yako. Lakini Mungu hataki kuwa “bosi” wako tu au “dikteta anayetawala maisha yako.” Anataka uhusiano wa karibu Zaidi nawe. Mungu hutumia picha ya familia kueleza uhusiano wa karibu ambao anataka kuwa na nao kwako.

**2 Wakorintho 6:18 Neno : Biblia Takatifu)**

**Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi.**

Mungu anataka kuwa baba mwenye upendo katika maisha yako. Ikiwa ulilelewa nyumbani na baba ayliyekuwa mwingi wa fadhili na upendo, huenda isiwe vigumu kwako kuelewa dhana hii ya Mungu kuwa kama baba yako wa hapa duniani, lakini ni bora zaidi.

Lakini kwa Wakristo wengi wapya hii "dhana ya baba" ni shida. Kulinganisha Mungu Baba na baba yao wa kidunia ni kichocheo cha kumbukumbu nyingi zenye uchungu. Kwa wengi, baba yao ni mgeni kwao. Wengine walikuwa na baba ambaye hakuwepo, au alikuwa mkali, kihisia hakuwepo, alikuwa mwenye ubinafsi, au mpinzani.

"Baba yangu aliondoka kwetu nyumbani wakati nikiwa mdogo sana," Jessie alisema. Mama yangu aliolewa tena, na baba yangu wa kambo alinidhilumu kingono kwa miaka mingi. Wakati unyanyasaji wake hatimaye ulifunuliwa, alikamatwa. Ilibidi nitoe ushahidi mahakamani. Mama yangu alikuwapo pia, lakini hakuwepo kwa ajili yangu. Alikuwa amekaa na baba yangu wa kambo.

Erick alikuwa na baba ambaye kamwe hakutosheka naye wala kumthamini. "'Hautaambulia chochote!' Ndiyo maneno ambayo baba alikuwa anayesema mara kwa mara," Erick anasema. "Maneno yalipenya kabisa ndani ya moyo wangu, na kwa sasa baada ya miaka mingi, bado nahisi uchungu kila wakati ninapoyasikia akilini mwangu."

Jessie na Erick wanawakilisha vijana wengi siku hizi ambayo wamekuwa na baba aliyewadulumu. Wawe walidhulumiwa kimapenzi au kimwili, dhana yao ya "baba" imeharibika. Badala ya kuwa na taswira chanya akilini mwao kuhusu "baba" inaunda picha ya nguvu iliyojaa usaliti, dhuluma, na uchungu kama kiwakilishi cha dhana ya 'baba'.

Je, mtu awezaje kushinda haya mawazo machungu ya "baba" na kukuza uhusuiano wa karibu na Mungu. Munugu ni wa kweli, na twapaswa kukumbatia ukweli huu, na kuishi katika ukweli wake licha ya shida amabazo ni mojawapo ya maisha yetu yaliyopita.

Ikiwa wewe ni mmoja wa wale ambaye wamekuwa na uhsuiano hasi na baba yao, basi fahamu kwamba Mungu anataka upate maana halisi ya kuwa na baba mwenye upendo ambaye hukuwa naye hapo awali. Atakuwa kuwa huyo baba kwako.

Bibilia imejaa maandiko yaliyo na uhusiano wa karibu ambao watu walikuwa naokwa Mungu. Zaburi 23 ni picha nzuri ya Mungu kama mchungaji wangu, iliyoandikwa na Daudi ambaye alikuwa mchungaji kabla ya kuwa mfalme. Hapa kuna njia kadhaa ambazo Mungu anataka uwe na uhusiano naye. Orodha hii yaweza kuwa ndefu Zaidi.

Ananipenda. Yohana 3:16

Ananijua kwa undani kabisa. Mathayo 6:25-28

Ananijali. Luka 12:22-28

Ananionyesha heshima na upendo.

Hanilazimishi kumtii

Hunipa muongozo. Yohana 14:26

Hunipa nguvu ya kumtii. Wafilipi 4:13

Hunisaidia wakati nina shida. 1 Wakorintho 10:13

Ni mungwana. Zaburi 86:15

Hunisamehe ninapofeli. 1 Yohana 1:9

Ni mvumilivu. 2 Petro 3:9

Huninidhamisha ninapokosa kumtii. Waebrania 12:5-11

Katika kukuza uhusiano huu wa kibinafsi na Mungu, twapaswa kujenga uelewa wa kibinfasi naye ambao ni wa kina. Huu sio uhusiano wa watu wawili walio sawa. Mungu ndiye mtawala- Ndiye kiongozi. Sisi ni wafuasi.

## B. Je, utii una nafasi gani katika uhusiano wangu na Mungu?

Ni nini maana ya kuwa na uhusiano mwema na Mungu — au na watu wengine? Katika ulimwengu wetu wa leo, mahusiano yasiyofaa yanaonekana kuwa ya kawaida kuliko yale mema. Machafuko ya kutoka familia yako yanaweza kuonekana “ya kawaida” kwako.

Kwa hivyo ni nini kitakachokusaidia kuyaondokea machafuko yako ya “kawaida” ya zamani na kukuza uhusiano wa karibu na wa kibinafsi na Mungu? Hatua moja muhimu ni kuelewa mipaka nasheria, ambazo Mungu ameweka ili kutusaidia.

Ungekuwa na mtoto wa miaka 2, ungeweka mipaka ya kumfanya mtoto wako awe salama. Ikiwa mtoto wako angetaka kwenda kucheza barabarani utamkatasa na kusema “Hapana,” hata akilia. Wewe unajua hatari iliyopo hata ingawa mtoto hajui.

Vivyo hivyo, Mungu ameweka mipaka ili kutulinda. Sheria zake hazitunyang’anyi uhuru, zinatoa mipaka salama ambayo tunaweza kufuruhia uhuru ambao Mungu ametupatia.

### 1. Sheria za Mungu

Kwa kuwa Mungu ndiye Kiongozi, tunahitaji kujua ni sheria zipi ambazo ametupatia maishani. Hili ni muhimu sana kwa Wakristo wapya kwani wengi hawajapata mafunzo yoyote kuhusu kile Mungu anatarajia kutoka kwao. Sheria ambazo Mungu ametupatia tuzitii zimeandikwa wazi katika Biblia.

Baadhi ya sheria maarufu zaidi ni Amri 10, zinazopatikana kwa kitabu cha Kutoka 20. Unapoangalia sheria hizi, zilizoandikwa maelfu ya miaka iliyopita, bado ni muhimu sana kwa leo. Sheria za “Usiibe,” na “usiue” sio kwa Wakristo tu, bali pia ni sheria za nchi yetu.

Unapoangalia amri 3 za kwanza, zinazingatia uhusiano wako wa kibinafsi na Mungu.

Kuna mtu ambaye amehesabu sheria zote katika Biblia na kupata zaidi ya sheria 600. Watu wengi katika Agano la Kale walizingatia tu sheria, na sio uhusiano wa kibinafsi na Mungu. Mungu anatafuta zaidi ya “watunza sheria.” Anataka uhusiano wa kibinafsi na wewe. Na njia moja wapo ya kuonyesha unataka uhusiano wa kibinafsi na Mungu ni kumtii.

### 2. Sheria kuu za Mungu

Siku moja mtu ambaye alikuwa mtaalam wa sheria ya Agano la Kale alimwendea Yesu na kumuuliza ni zipi sheria kuu katika Biblia.

**Mathayo 22:35-40 Toleo la Kimataifa**

**35Mmoja wao, mtaalamu wa Sheria, alimjaribu kwa kumwuliza: 36 "Mwalimu, amri kuu ni ipi katika Sheria?" 37Yesu akajibu: "'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili yako yote.' 38 Hii ndiyo amri ya kwanza na kuu. 39Na pili ni kama hii: 'Mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.' 40Sheria zote na Manabii hutegemea amri hizi mbili."**

Jibu la Yesu linatupatia mtazamo wenye nguvu juu ya kile Mungu anafikiria kuhusu sheria zote katika Biblia. Sheria kuu inazingatia uhusiano wa kibinafsi naye. Kuwa Mkristo aliyefanikiwa hakuhusiani kwa vyovyote na utajiri au nguvu yako, au mahusiano ya kifamilia. Kulingana na Mungu kila Mkristo ana uwezo wa kufanikiwa kwa kutii sheria kuu zaidi katika Biblia. Umri au akili, au ukosefu wake, hauhusiani na sheria hii. Yote ni kuhusu upendo.

Sheria hii kuu zaidi katika Biblia inatuelekeza kwa uhusiano mkuu kati ya kumpenda na kumtii Mungu.

## C. Kwa nini umtii Mungu?

Utiifu na upendo na viwili vilivyo na uhusiano wa karibu sana poja kwa lingine. Vyote viwili vina ushawishi mkubwa kwa kila mmoja. Ikiwa utamtii Mungu, lazima ujifunze kumpenda. Ni ndani tu ya uhusiano wa kibinafsi unaotegemea upendo kwa Mungu ndipo utagundua hamu na nguvu ya kutii sheria za Mungu. Upendo ndio msingi ambao utifu hujengwa juu yake. Kadiri upendo wako kwa Mungu unavyozidi kuwa mkubwa, ndivyo itakavyokuwa rahisi kumtii.

Kila wakati tunapotii moja ya sheria Zake, matendo yetu huwa yanamwambia Mungu, "Ninakupenda." Kutii sheria za Mungu ndiko kunakofanya upendo kuwa safi na mzuri. Upendo bila utiifu husababisha uchafu, ubinfasi, na uharibifu. Upendo hugeuka kuwa tamaa mtu anapokosa kumtii Mungu.

### 1. Mungu ni Upendo

Mistari mingi katika Biblia inazungumza juu ya upendo wa Mungu. Mungu huyu mwenye upendo anamjali sana kila mtu, awe mdogo au mkubwa.

Tunapochagua kumtii Mungu, basi tunachagua kumtii Mungu mwenye upendo. Hatungeweza kufanya chaguo salama zaidi kuliko kumtii Mungu. Haa dosari yoyote. Ni mkamilifuMungu huyu mwenye upendo anatutaka tumtii yeye.

**1 Yohana 3:16 (Biblia Takatifu)**

**Tunajua upendo wa kweli ni nini kwa sababu Kristo alitoa maisha yake kwa ajili yetu. Kwa hivyo pia tunapaswa kutoa maisha yetu kwa ajili ya ndugu na dada zetu Wakristo.**

**2 Wakorintho 13:11 (Biblia Takatifu)**

**Ndugu na dada wapendwa, ninafunga barua yangu kwa maneno haya ya mwisho: Furahini. Badili njia zako. Tutiane moyo. Ishi kwa amani na amani. Ndipo Mungu wa upendo na amani atakuwa pamoja nawe.**

### 2. Mungu anakupenda

Yohana 3:16 inatuambia kwamba Mungu anapenda ulimwengu wote na wala si watu wachache tu. Anakupenda sana. Maisha yako ya zamani ya dhambi hayamzuii kukupenda. Wewe ni wa kipekee kwake.

**Yohana 3:16 (Biblia Takatifu)**

**Kwa Maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimengu hata akamtoa mwanawe wa Pekee illi yeyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.**

### 3. Mungu alikwambia umpende

Sheria muhimu zaidi katika Biblia nzima ni kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, akili, roho na nguvu zako zote. (Tazama Mathayo 22:37 na Marko 12:30.) Kwa maneno mengine, tumeamriwa kumpenda Mungu na kila kitu tulicho nacho. Tunapaswa kumpenda Mungu kuliko mtu mwingine yeyote.

Yesu anazungumzia uhusiano huu kati ya upendo na utiifu.

**Yohana 14:15 (Biblia Takatifu)**

**Ikiwa mnanipenda, zingatieni amri zangu.**

Yesu alisema ikiwa unampenda, utatii sheria za Mungu. Usipomtii Mungu, hii inaonyesha kuwa haumpendi Mungu. Ikiwa haumpendi Mungu, utaona haiwezekani kutii sheria zake.

## D. Ninawezaje kutii sheria kuu ya Mungu?

### 1. Ninaweza kuanza vipi kumpenda Mungu?

Unawezaje kutii sheria kuu ya Mungu? Unaweza kufanya nini kumwonyesha Mungu kwamba unampenda? Kuna njia kadhaa za vitendo kwako za kuonyesha Mungu kwamba unampenda. Hapa kuna chache. Labda unaweza kuongeza maoni yako mwenyewe.
Soma 1 Wakorintho 13 ili uone njia zaidi za kuonyesha upendo wa kweli. Unaposoma Biblia yako kila siku, tafuta mifano ya watu katika Biblia ambayo inaonyesha jinsi walivyompenda Mungu kupitia utiifu wao.

1. Tii sheria za Mungu
2. Tii kanuni zilizo nyuma ya sheria za Mungu
3. Mpe Mungu haki zako za kibinafsi

4. Fanya kile Mungu anataka ufanye
5. ___________________________________
6. ___________________________________
7. ___________________________________
8. ___________________________________

Tunapaswa kutafuta njia rahisi, za vitendo vya kumwonyesha Mungu kwamba tunampenda tunapofanya shughuli zetu za kila siku. Tafuta fursa hizo wakati wa maamkuli, ukiwa kazini, darasani, wakati wa burudani, mapupumziko, na ukiwa kanisani.

Luka 6:27-38 ina orodha nyingine ya njia za kuonyesha upendo kupitia kwa matendo. Unaweza kujadili jinsi unaweza kuanza kujaribu baadhi ya njia hizi maishani mwako. Hapa kuna mambo machache zaidi yaliyoorodheshwa na darasa la Wakristo wapya.

1. Uliza ushauri kwa Mungu.
2. Mshukuru kwa msaada Wake.
3. Mwabudu Yeye.
4. Fikiria juu ya Mungu kuwa pamoja nami.
5. Onyesha mitazamo ya kibiblia.
6. Mtolee Mungu.

Jambo kuu hapa ni kutafuta njia yako ya kujifunza kumpenda Mungu. Kukuza uhusiano wa kina wa kibinafsi na Mungu kunaweza kuchukua muda, lakini unahimizwa kuendelea kukufanyia kazi.

## 2. Je, itakuwaje ikiwa sina nguvu ya kumtii Mungu?

Unaweza kusema, “Sina uwezo wa kumpenda Mungu au kutii amri zake. Mimi ni dhaifu sana.” Mungu anajua udhaifu wako kuliko wewe unavyoujua, na bado anakupenda. Na amekupa ahadi mbili maalum.

**2 Timotheo 1:7 (Biblia Tatakatifu)**

**Kwa maana Mungu hakutupa roho ya woga na hofu, lakini ya nguvu, upendo, na nidhamu ya kibinafsi.**

**2 Wakorintho 12:9 (Biblia Takatifu)**

**Lakini yeye (Mungu) aliniambia, “Neema yangu inakutosha, kwa maana nguvu zangu hukamilishwa katika udhaifu.” Kwa hivyo nitajisifu zaidi kwa furaha juu ya udhaifu wangu, ili nguvu ya Kristo ikae juu yangu.**

Ahadi hizi zote mbili zinatoa tumaini kubwa kwako. Ikiwa unasema, “Siwezi kumpenda mtu huyo,” au “Siwezi kumpenda Mungu,” usijali. Mungu atakupa upendo, ili uweze kumpenda yeye na wengine. Kwa kweli 2 Timotheo 1:7 inakitaja kama kitendo kilichofanyika tayari - Mungu ametupatia karama hizi.

Ahadi ya 2 Wakorintho 12:9 inazungumzia wale ambao wanakabiliwa na shida- wale ambao ni dhaifu. Mungu anaahidi kutupatia nguvu zote tunazohitaji - nguvu ya kupenda, na nguvu katika kila eneo la maisha yetu. Lakini ni zaidi ya nguvu ya kumtii Mungu. Inachukua shauku ya kibinafsi ya kutii — inayotoka ndani kabisa ya moyo wako.

### 3. Na je, iwapo sihisi upendo wowote kwa Mungu?

Katika ulimwengu wetu wa leo, upendo mara nyingi huelezewa kama hisia. Labda umemsikia Mkristo akisema, “Ninahisi kumpenda Yesu sana. Ninahisi kama moyo wangu utalipuka!” Je, unaweza kujihusisha na mtu huyo? Au wewe ni kinyume? Unamtazama mtu huyo, na kwa utulivu useme, “Huyo ni mtu wa ajabu!”

Au labda uliwahi kuhisi kuwa karibu sana na Mungu, lakini sasa hisia hizo zimekwisha. Labda uliamka asubuhi moja lakini msisimko huo wote ulikuwa umetoweka.

Amri kuu katika Biblia haikuamuru kuwa na hisia fulani. Upendo ni zaidi ya hisia-ni kujitolea, ni chaguo. Upendo wa kweli hauamuliwa sana na jinsi unavyohisi, lakini ni kupitia kwa matendo yako. Upendo wa kweli huonyeshwa kwa vitendo vya upendo ambavyo hutoka kwa moyo safi.

Wakristo wengi wapya kwa kweli hung’ang’ana na wazo la kumpenda Mungu wasiyemwona. Kujifunza kumpenda Mungu kwanza huanza kwa kujifunza kumtii. Kwa vitendo rahisi vya utii, utaanza kuona mabadiliko katika moyo wako na kuanza kuhisi upendo kwa Mungu. Kunaweza kuwa kwa haraka katika uhusiano wako, au hisia za kumpenda Mungu zinaweza kuja polepole.

Lakini kumbuka tu, hisia huja na kuondoka. Hiyo haimaanishi upendo huja na kutoweka kwa sababu kwamba hisia hubadilika. Hata katika siku ambazo hisia za upendo kwa Mungu zimepita, bado unaweza kuchagua moyoni mwako kusema, “Ninachagua kumpenda Mungu na kuuonyesha kwa matendo yangu.”

Ikiwa unamtii Mungu tu wakati unahisi kutaka kumtii Yeye, basi unaelekea kwenye shida. Kuchagua kumtii Mungu lazima kutoke moyoni — kujitolea kabisa kutoka ndani ya moyo wako kumtii Mungu bila kujali unahisi vipi.

Jambo lingine zaidi—wakati unapompenda mtu, wewe hutaka kuongea naye. Kadri unavyoongea na Mungu kila siku, ndiyo utakvyozidi Kumjua na ndivyo utakavyohisi Kumpenda hata zaidi.

## E. Je, nia za mtu huwa na nafasi gani katika kumtii Mungu?

Mtoto mdogo anapoanza kujifunza juu ya utii, yeye huwa ni mchanga sana kuelewa swala la nia. Wao hufunzwa kutii – kikomo — “kwa sababu nilisema hivyo!” Sheria zimewekwa na wazazi, na wazazi wanazisimamia kwa sababu wanataka kumlinda mtoto wao.

Lakini wakati mtoto anakua hadi kufikia kubalehe, kiwango kipya cha utii kinahitajika. Mtu mzima huyu anayeibuka anahitaji kujifunza sababu za kina zaidi za sheria, na athari zao kwa sheria hizo. Sasa kijana ana uchaguzi wa kufanya hapa, maamuzi ambayo yanajumuisha nia.

Mungu anataka umtii, na ameahidi kukupa nguvu unayohitaji kufanya hii. Lakini hatakulazimisha kutii. Lazima uchague. Kwa hivyo ni nini kitakusaidia kufanya chaguo sahihi? Ni nia zako.

## 1. Nia ni nini?

Mara nyingi tunasikia neno “nia” lakini linamaanisha nini haswa? Hapa kuna majibu ya kibinafsi yaliyotolewa na wengine. Labda una kitu kingine cha kuongeza kwenye orodha hii.

1. Kusudi
2. Sababu kuu ni kwa nini nafanya kitu fulani
3. Tamaa
4. Nguvu au wazo ambalo linanihimiza kufanya kitu
5. Wazo lililo nyuma ya hatua unayochukua

Watu wanaweza kuwa na nia tofauti nyuma ya matendo yao yote, sio tu matendo yao ya utii. Mtu anaweza kuchochewa na woga, hatia, wajibu - nina deni lako - ni wakati wa kulipwa, au ujanja. Au kunaweza kuwa na nia nzuri: fadhili, wasiwasi, wajibu, upendo, huruma, shukrani, au furaha tu ya kutoa.

## 2. Nia yangu ya kumtii Mungu ni gani?

Kwa hivyo ni nini kinachokutia motisha wa kumtii Mungu? Woga wa kwenda kuzimu? Hilo linaweza kufanya kazi kwa muda mfupi. Lakini unahitaji nia nzuri kuliko hofu ya kwenda kuzimu ili kukufanya upendane na Yesu.

Ni nini kitakachokufikisha mahali ambapo unasema, “Nataka kumtii Mungu.” Nia iliyo nzuri ya kumtii Mungu ni nia ya upendo.

Lakini utajuaje ikiwa kitendo cha mtu ni kitendo cha upendo, au dhuluma? Jibu ni “nia yako.” Kitendo ambacho ni tendo la upendo daima huwa na nia yake ya kuonyesha upendo.

Watu wawili wangeweza kufanya kitu kimoja, lakini wana nia tofauti. Kitendo ambacho ni tendo la upendo katika kesi moja kinaweza kuwa kitendo cha ubinafsi katika kesi nyingine. Tofauti muhimu ni nia ya mtu.

Kila mmoja wetu huchagua nia zatu. Pengine hapo zamani ulifanya kitu kwa nia mbaya. Sasa kwa msaada wa Mungu unaweza kuanza kumtii Mungu na kuwa na hamu ya kumwonyesha upendo.

**Mithali 21:2 (Biblia Takatifu)**

**Tunaweza kuhalalisha kila tendo lakini Mungu anaangalia nia zetu.**

**Mithali 20:27 (Biblia Takatifu)**

**Dhamiri ya mtu ni mwangaza wa Bwana, akifunua nia zake zilizofichwa.**

Mistari hii miwili inatuonyesha wazi kuwa Mungu daima anajua nia zetu. Tunaweza kuficha nia zetu kutoka kwa watu wengine, lakini si kwa Mungu. Changamoto tunayokabiliana nayo leo hii ndiyo itakuwa alama za uhusiano wetu mpya na Mungu. Je, upendo utakuwa nia yetu? Je, utii kwa Mungu utakuwa shauku ya mioyo yetu?

Kuna mengi zaidi kuhusu kumjua Mungu kuliko kumtii Yeye. Lakini hakika hakika hiyo ni hatua moja kuu ya kuanzisha uhusiano wa kibinafsi na Yeye. Je, mitazamo yetu inaathiri vipi uwezo wetu wa kumtii Mungu? Huo ndio mkazo wa Sura inayofuata ya 2.

# Sura 2
# Mitazamo na Utiifu

Tumejadili ni kwa nini tunapaswa kumtii Mungu. Tunaona kwamba sheria kuu ya Mungu inazingatia upendo. Sasa hebu tuangalie kwa karibu jinsi mitazamo yetu inavyoathiri tabia zetu.

Jambo kuu la sura hii ni kwamba tunahitaji kuwa na mitazamo ya utifui kwa Mungu ikiwa tutamtii Mungu kila wakati. Kwa hivyo unajuaje ikiwa una mitazamo ya utiifu kwa Mungu?

Inaweza kuwa rahisi kuona mitazamo hii ikiwa kwanza utaangalia jinsi unavyowaitikia watu wengine katika maisha yako leo - haswa viongozi au wale walio katika nafasi za mamlaka. Ikiwa unajikuta ukiitikia kwa mitazamo ya kutotii watu wengine, basi labda unahitaji kuangalia kwa makini kuona iwapo jambo hilo pia ni shida kwa uhusiano wako na Mungu.

Somo hili linaweza kutumiwa kwa urahisi kwa viongozi wetu wote - Mungu na viongozi wetu wa kidunia. Lakini lengo letu kuu ni kuangalia jinsi mitazamo yetu kwa sheria za Mungu inavyoathiri utii wetu kwa sheria zake.

## A. Angalia mitazamo inayofanya iwe rahisi kutomtii Mungu

Mtazamo ni njia fulani ya kufikiria, kutoa maoni, mtindo wa kuwaza.

Mojawapo ya sababu ambazo ni kwa nini watu wana wakati mgumu kumtii Mungu ni kwa kuwa wana mitazamo mibaya kwake. Unaweza kuuliza, “Je, Mitazamo yangu ina uhusiano gani na uwezo wa kumtii Mungu?” KWA NJIA KUBWA! Unachofikiria juu ya Mungu kitaathiri sana jinsi unavyomtii.

Tazama iwapo una mitazamo yoyote kwa Mungu.

______Mtazamo wa kushutumu

______Mtazamo wa uasi

______Mtazamo wa kutoshukuru

______Tabia ya uvivu

______Mtazamo wa kinyongo

______Mtazamo wa ukaidi

Je, mtu anaonyeshaje kwamba ana moja au zaidi ya mitazamo hii kwa Mungu? Kuna njia nyingi-kwa kile unachosema, unachofanya, jinsi unavyoitikia wakati Mungu anakuambia ufanye kitu, nk.

Sisi huwa tunaonyesha mitazamo hii tunapokabiliwa na hali inayohusisha moja ya sheria za Mungu. Kwa mfano, ikiwa utajaribiwa kuiba kitu, jinsi utakavyojibu itaamuliwa na mitazamo uliyonayo kwa hali hiyo.

Na tufikirie kwamba msimamizi wa duka amempa mama yako wakati mgumu sana wakati alipojaribu kutafuta bidha fulani. Ndani ya moyo unamkasirikia sana meneja kwa yale aliyomtendea mama yako. Dakika chache baadaye unaona maji ya machungwa kwenye chupa na mara mawazo yanaingia kichwani mwako, “ Ni kwa nini nisichukue hizi kadhaa ili nilipize kisasi kwa huyu meneja mbaya.”

Ukiruhusu mtazamo wa kinyongo kuamua majibu yako, basi unaweza kujaribu kuiba maji ya machungwa. Mtazamo mbadala wa kuitikia swala hili ungekuwa ni kumsamehe yule msimamizi na kuondoa kwa haraka mawazo ya kuiba akilini mwako kama njia ya kulipiza kisasi kwa tabia yake mbaya.

### Mfalme Sauli na tabia yake ya uasi

Hadithi katika 1 Samweli 15 inaonyesha Mfalme Sauli na tabia yake ya uasi. Je, tabia yake na maneno yake yalifunuaje tabia zake za kutotii? Mungu anaweka wazi kabisa anachofikiria juu ya mitazamo ya kutotii.

**1 Samweli 15:22-23 (Biblia Takatifu)**

**Lakini Samweli akajibu, “Ni nini kinachompendeza BWANA: sadaka zako za kuteketezwa na dhabihu, au kutii kwako sauti yake? Utii ni bora kuliko dhabihu. Kumsikiliza ni bora zaidi kuliko kutoa mafuta ya kondoo waume.**
**23 Uasi ni mbaya kama dhambi ya uchawi, na ukaidi ni mbaya kama kuabudu sanamu. Kwa sababu umelikataa neno la BWANA, naye amekukataa wewe usiwe mfalme.”**

Mungu huona mtazamo wa uasi kuwa mbaya kama dhambi ya uchawi. Yeye huona mtazamo wa ukaidi kuwa mbaya kama tendo la kuabudu sanamu.

Unaweza kuuliza, “Ninawezaje kuondoa mitazamo hii?” Jibu liko wazi — lakini si rahisi. Badilisha mtazamo usiofaa kwa mitazamo ya utii.

Tazama kozi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* inayoitwa **Mitazamo** kwa habari zaidi jinsi ya kuondoa mitazamo mibaya na njia za kukuza mitazamo mipya.

## B. Kuza mitazamo ya utiifu

Mojawapo ya sehemu muhimu zaidi ya kujifunza jinsi ya kumtii Mungu ni kukuza mitazamo ya utiifu. Wafilipi 2:5 inatuambia tuwe na nia zile zile alizokuwa nazo Kristo. Alikuwa mtiifu hadi kwa kifo chake cha uchungu pale msalabani. Unaposoma vitabu vinne vya kwanza katika Agano Jipya, unaona Yesu akijibu kwa utii ambao unadhihirisha kwa nguvu sana mitazamo ya utii aliyokuwa nayo. Shauku yake ya kumpendeza Mungu ilikuwa muhimu sana maishani mwake.

**Yohana 5:19-20 (Biblia Takatifu)**

**Yesu akamjibu, “Nakuhakikishia, Mwana hawezi kufanya kitu peke yake. Yeye hufanya tu kile anachomwona Baba akifanya. Chochote Baba hufanya, Mwana pia hufanya. [20] Kwa maana Baba anampenda Mwana na humwambia yote anayofanya.”**

Tunapokuwa na mitazamo ya utii, ni rahisi zaidi kutii sheria za Mungu. Kukuza mitazamo ya utii inaweza kuchukua muda. Labda njia yenye nguvu zaidi ya kujenga mitazamo ya utii ndani ya maisha yako ni kukariri maandiko ambayo yanazungumzia maswala haya.

Je, Yesu alikuwa na mitazamo gani ya utii katika maisha yake? Hizi ni tabia zile zile ambazo anataka tuendeleze katika maisha yetu leo.

## 1. Mtazamo wa heshima

### a. Mtazamo wa heshima ni nini?

l) Heshima inamaanisha heshima iliyochanganywa na upendo. Heshima yangu kwa Mungu imechanganywa na upendo Kwake. 1 Petro 2:18

2) Kupendezwa i-napedezwa na Mungu. Ninamtazama Mungu kwa heshima. Ninamheshimu.

### b. Ninawezaje kukuza tabia ya heshima?

1) Ninaelewa kuwa Mungu anafanya kazi katika maisha yangu kupitia viongozi wangu.

**Waebrania 13:17 (Biblia Takatifu)**

**Watiini viongozi wako na utii kwa mamlaka yao. Wanakuangalia kama wanaume ambao wanapaswa kutoa hesabu. Watii ili kazi yao iwe ya kufurahisha, na sio mzigo, kwani hiyo haitakuwa na faida kwako.**

2) Ninatambua kuwa Mungu anatumia viongozi wangu kunifanya niwe mtu ambaye Yeye (Mungu) anataka niwe.

**Mithali 21:1 (Biblia Takatifu)**

**Moyo wa mfalme uko mkononi mwa Bwana; anauelekeza kama mto popote apendapo.**

3) Ninawatazama viongozi wangu kama “mikono ya Mungu,” wakiniongoza na kunielekeza.

# 2. Mtazamo wa mtumishi

## a. Mtazamo wa mtumishi ni nini?

l) Kuelewa kuwa mimi sio bosi wangu mwenyewe.

2) Natambua kwamba ninamtumikia Mungu ninapowawafanyia kazi viongozi wangu.

**Wakolosai 3:23 (Biblia Takatifu)**

**Fanya bidii na kwa moyo mkunjufu kwa chochote unachofanya, kana kwamba unafanya kazi kwa Bwana kuliko kwa watu.**

3) Hii inamaanisha mimi ni kazi ya idhini ya Mungu katika kila kitu ninachofanya, haswa kwa kumtii Mungu na viongozi wangu.

## b. Ninawezaje kukuza mtazamo wa mtumishi?

l) Ninajitoa mwenyewe kwa Mungu na viongozi wangu na kuwatii.

**1 Petro 2:18 (Biblia Takatifu)**

**Ninyi mlio watumishi mtawanyenyekea mabwana wenu kwa heshima inayostahili — si kwa wema na wema tu, bali hata kwa walio wagumu.**

2) Ninajiweka chini ya ulinzi wa Mungu.

3) Ninatafuta njia za kumfanya mtu mwingine afanikiwe, haswa viongozi wangu. Ninafurahi juu ya hii na kupata furaha ya kweli kwa kufanya hivi.

4) Sijaribu kufanya kazi ya Mungu. Sijaribu kuchukua majukumu yake.

# 3. Mtazamo wa shukrani (nia ya shukrani)

## a. Mtazamo wa shukrani ni nini?

1) Kushukuru kwa kuwa na Mungu kama kiongozi wangu.

2) Kuwa na furaha ya kweli na kuthamini kile Mungu anataka kunifanya niwe ndani ya mtu Anayetaka niwe.

### b. Ninawezaje kukuza mtazamo wa shukrani?

l) Nahitaji kujifunza kuwa na furaha kwa kuwa na Mungu kama kiongozi wangu. Namshukuru Mungu kila siku kuwa mimi ni mtoto wake.

**1 Wathesalonike 5:18 (Biblia Takatifu)**

**Haijalishi ni nini kitatokea, siku zote shukuru, kwa maana haya ni mapenzi ya Mungu kwako wewe uliye Kristo Yesu.**

2) Onyesha shukrani za kweli kwa Mungu kila siku. Nitamshukuru kila wakati anapotumia watu wengine kunishauri au kunisahihisha.

3) Nampa Mungu matarajio yangu yote. Andika orodha ya mambo yote ninayotarajia atanifanyia. Kisha omba na umpe Mungu matarajio haya yote.

## 4. Mtazamo wa utulivu

### a. Je, mtazamo wa utulivu ni nini?

l) Ni rahisi sana-jifunze jinsi ya kuwa kimya. Kujifunza kuwa kimya katika kile ninachosema, katika maeneo mawili, (l) kiasi cha maneno ninayosema, na (2) kwa nguvu gani ninasema.

2) Kujifunza kuwa kimya kwa *ndan*i na hata nje.

3) Kujifunza kuwa na amani na Mungu.

**1 Petro 3:4 (Biblia Takatifu)**

**Uzuri wako unapaswa kutoka ndani. Unapaswa kutoka moyoni. Hii ndio aina ambayo hudumu. Uzuri wako unapaswa kuwa roho ya upole na utulivu. Mbele ya Mungu hii ina thamani kubwa na hakuna kiwango cha pesa kinachoweza kuinunua.**

Aya hii imeandikwa kwa wake kuhusu mitazamo yao kwa waume zao. Walakini, kanuni hiyo ni nzuri kwa kila mtu-kukuza tabia ya utulivu. Mungu anachukulia hii kama kitu cha thamani sana.

### b. Ninawezaje kukuza mtazamo wa utulivu?

l) Nahitaji kujifunza kumtii Mungu bila kudai kujua sababu zake zote. Ninahitaji kuwa tayari kutii kwa sababu niliambiwa nifanye hivyo.

2) Naweka tumaini langu kwa Mungu, kwamba ataweza kufanya kazi kupitia viongozi wangu na kwamaisha yangu kufanya kile anachotaka. Natumaini Mungu kufanya hivi hata kama viongozi wangu watafanya makosa na kufanya mambo vibaya. Hivi ndivyo Yesu alivyofanya mambo.

**1 Petro 2:23 (Biblia Takatifu)**

**Hakulipa kisasi alipotukanwa. Wakati aliteseka, hakutishia kupata kisasi. Aliacha kesi yake mikononi mwa Mungu, ambaye siku zote huhukumu kwa haki.**

3) Sitapingana na Mungu.

4) Sitaki ufafanuzi wa ni kwa nini nifanye kitu kabla ya kutii.

Unapochunguza maisha ya Yesu, utagundua kuwa Alikuza tabia hizi za utii katika maisha yake. Alionyesha mitazamo hii katika uhusiano Wake na Mungu na na viongozi Wake wa kidunia. Kuna mitazamo mingine ya utii ambayo inaweza kuorodheshwa hapa, lakini hii inakupa mwanzo mzuri.

Unapojitahidi kukuza tabia hizi nne za utii, itakuwa rahisi kumtii Mungu. Utagundua pia unapojitahidi kukuza tabia hizi za utii unaweza kuanza kusukuma mitazamo ya kutotii nje ya maisha yako. Ni mchakato — ukibadilisha mitazamo ya kutotii na kuitii. Swali ni-nini kiko moyoni mwako? Je, unataka kumtii? Ikiwa kweli unataka kumtii, atakusaidia.

Tabia hizi za utii pia huzungumza na suala lingine—zinaashiria “utiifu wenye hekima”. Utiifu wa kweli wa kiroho si utii wa pofu – utii usio na fikira. Yesu alikuwa mtiifu kabisa kwa Mungu na sheria zake. Alichagua kufanya hivi. Maisha yake yanaweza kutambuliwa kama “utiifu wenye hekima”. Watu wenye hekima watafuata mfano wa Yesu.

# Sura ya 3
# Ni sheria zipi nina paswa kutii?

Ikiwa unataka kuanza mjadala mkali, basi uliza maswali haya matatu yaliyo hapa chini. Usishangae ikiwa utawakuta Wakristo wakiwa na maoni tofauti sana kuhusu maswali haya matatu.

(1) Je Wakristo ni lazima watii sheria zote za Mungu ambazo ziko katika Agano Jipya?

(2) Je, Wakristo ni lazima watii sheria zote za Mungu zilizo katika Agano la Kale?

(3) Ikiwa Wakristo hawapaswi kutii sheria zote za Mungu kwenye Biblia, unaamuaje ni sheria gani za kutii na ni zipi za kupuuza?

Swali hili la mwisho haswa huibua maswala magumu. Je sisi kwa kweli huamua kuchagua ni sheria zipi tutatii? Je, ni wapi ambapo Mungu anasema tunaweza kupuuza sheria fulani katika Biblia?

Ikiwa unachukua msimamo kwamba tunapaswa kutii sheria zote za Mungu, basi soma sheria zifuatazo za Agano la Kale. Je, unatii sheria hizi? Ikiwa sivyo, kwa nini?

**Mambo ya Walawi 11:26-27 (Biblia Takatifu)**

**Mnyama yeyote aliyegawika kwato lakini hana kwato au ambaye hacheu kutafuna ni najisi kwako. Ukigusa maiti ya mnyama kama huyo, utakuwa unajisi mpaka jioni. 27Kwa wanyama wanaotembea kwa miguu minne, wale walio na makuchani najisi kwako. Ukigusa maiti ya mnyama kama huyo, utakuwa unajisi mpaka jioni.**

(Hii ni pamoja na wanyama wengi, wakiwemopaka, mbwa na sungura)

**Mambo ya Walawi 20:9-10 (Biblia Takatifu)**

**Wote wanaomlaani baba yao au mama yao lazima wauawe. Wana hatia ya kifo. 10Ikiwa mwanamume azini na mke wa mtu mwingine, lazima mwanamume na mwanamke wauawe.**

**Kumbukumbu la Torati 23:12-13 (Biblia Takatifu)**

**Tia alama eneo nje ya kambi kwa choo. 13 Kila mmoja wenu lazima awe na kijembe kama sehemu ya vifaa vyenu. Wakati wowote unapojisaida, lazima uchimbe shimo na jembe na kufunika kinyesi.**

# A. Aina za sheria za Mungu

Biblia ina aina tofauti za sheria. Baadhi ya sheria hizi zinaweza kuwekwa kwa urahisi katika vikundi pana. Hapa kuna aina nne kuu. Walakini, sheria zingine zinafaa kuwa kwa aina zaidi ya moja.

1. Sheria za afya
2. Sheria za serikali ya raia kwa taifa la Israeli
3. Sheria za dini
4. Sheria za maadili

Vikundi hivi vine vinaonekana kuwa rahisi, lakini kwa kweli, sheria zingine zinaweza kutoshea katika vikundi viwili. Kikundi cha mwisho—sheria za maadili—pia ni shida. Kwa kweli, kila sheria katika Biblia ina suala la maadili lililofungamanishwa nalo. Makundi haya manne yameundwa na mwanadamu. Hautapata kifungu katika Biblia ambacho kinavunja sheria hizi katika sehemu hizi nne.

Walakini, ni vyema kuona baadhi ya vikundi vikuu ambayo sheria hizi zinafaa wakati tunaziangalia kwa karibu.

## 1. Sheria za Afya

Vitabu vya Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu, na Kumbukumbu la Torati katika Agano la Kale vimejazaa sheria nyingi tofauti ambazo zinahusiana moja kwa moja na kudumisha afya njema. Kumbukumbu la Torati 23:12-13 iliyonukuliwa hapo juu ni mfano mmoja. Nyingi ya sheria hizi pia hutoa kanuni za kina kuhusu matibabu ya aina tofauti za magonjwa. S. I. McMillen, ambaye ni daktari wa matibabu, ameandika kitabu kizuri kiitwacho, **None of These Diseases** (Flemming H. Revell Publ. Co). Anaeleza usahihi wa matibabu wa sheria za Agano la Kale. Unaweza kusoma kitabu hiki kish ukaona jinsi sheria hizi zinavyofaa kitabibu leo.

## 2. Sheria za kiserikali kwa raia wa taifa la Israeli

Sheria nyingi katika vitabu vya Kutoka hadi Kumbukumbu la Torati zilipewa Wayahudi ili kuanzisha kanuni ya kisheria kwa taifa la Israeli. Huenda ni kati ya Wayahudi milioni moja na tatu walioondoka Misri chini ya uongozi wa Musa. Umati huu wa watumwa wa zamani ilibidi sasa uanzishe serikali ili kushikilia taifa lao jipya pamoja na kutoa uongozi na huduma zote zinazohitajika. Nyingi ya sheria hizi zilishughulikia jinsi ya kutatua migogoro, uuzaji na upangishaji wa ardhi, kutoza riba, utunzaji wa mayatima, n.k.

## 3. Sheria za dini

Sheria nyingi za Agano la Kale zilihusiana na mazoea ya dini ya Kiyahudi. Mafunzo na majukumu ya makuhani na Walawi, aina tofauti za dhabihu za wanyama na chakula, likizo ya kidini, haya ndiyo maswala makuu yanayoshughulikiwa na sheria hizi.

### 4. Sheria za maadili

Sheria za maadili za Mungu mara nyingi huelezewa kama zile sheria za wakati ambapo zinahusika na mahusiano ya watu. Amri Kumi (Kutoka 20:1-17) na sheria mbili kuu katika Biblia (Luka 10:27) ni mifano ya sheria za maadili za Mungu. Sheria za maadili za Mungu zinaweza kutiiwa katika utamaduni wowote, taifa, kipindi cha wakati, na mtu yeyote, bila kujali ni asili gani ya kiuchumi au elimu.

**Yakobo 1:25 (Biblia Takatifu)**

**Lakini yule ambaye anaendelea kuangalia Sheria kamilifu ya Mungu na asisahau hiyo atafanya kile inachosema na kuwa na furaha kama anavyofanya. Neno la Mungu huwafanya watu wawe huru.**

Kwa hivyo tumerudi kwa swali kuu-ni zipi kati ya sheria za Mungu ambazo Wakristo leo wanatakiwa kutii? Ni zipi ambazo hatuhitaji kutii leo?

## B. Mjadala kuhusu nisheria zipi tunapswa kutii leo

Mjadala kuhusu ni sheria zipi ambazo watu wapaswa kutii si ubishi mpya. Hata katika siku za Yesu, na katika kanisa la Agano Jipya baada ya Yesu kurudi mbinguni, kulikuwa na maoni tofauti. Lakini muda mrefu kabla ya hapo, tunaona maoni haya yanayopingana. Kwa kweli, mapambano yalianza kati ya Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni, Wakati Hawa aliamini kile shetani alichomwambia, kwamba angepuuza kile Mungu alikuwa amesema na kwa hakika angekuwa mtu bora.

**Mwanzo 3:1-5 (Biblia Tataktifu)**

**Nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa porini walioumbwa na Mwenyezi-Mungu. Basi, nyoka akamwambia huyo mwanamke, “Ati Mungu alisema msile matunda ya mti wowote bustanini?” Mwanamke akamjibu huyo nyoka, “Twaweza kula matunda ya mti wowote bustanini; lakini Mungu alisema, ‘Msile matunda ya mti ulio katikati ya bustani, wala msiuguse, msije mkafa.’” Nyoka akamwambia mwanamke, “Hamtakufa! Mungu alisema hivyo kwa sababu anajua kwamba mkila matunda ya mti huo mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.”**

Tukiangalia nyuma tunaweza kuoan kwamba Shetani alimdanganya Hawa na kumfanya aamini uongo. Matokeoa yake yalibadilisha ulimwengu katika nyakati zote. Mojawapao ya somo kuu ambalo tunapaswa kupokea kutokana na hali ya Adamu na Hawa ni umuhimu wa kumtii Mungu, na kutohadaiwa na Shetani am mtuyeyote yule.

Kwa hivyo tunapaswa kutii sheria gami katika maaandiko leo hii? Hata Wakristo waaminifu wana mawazo tofauti kuhusu sheria ambazo Wakristo wanapswa kutii leo hii. Hapa kuna muhtasari wa baadhi ya maaoni haya.

# Msimamo wa 1
# Wakristo leo hii wanapaswa kutii Sheria zote za Agano la Kale

Huu sio mtazamo amabao unashikiliwa na watu wengi, lakini Wakristo wengi wanasimama kwaa maneno ya Yesu kwamba hakuja kutengua sheria za Agano la Kale, bali kuzitimiza.

**Mathayo 5:17-19 (Biblia Takatifu)**

**[17] "Msidhani kwamba nimekuja kutangua Sheria au Manabii;**
**Sikuja kuyamaliza bali kuyatimiza. [18] Kweli nawaambieni, mpaka mbingu na dunia zitakapoondoka, hata herufi moja ndogo, hata alama yoyote ya wino, hazitapotea kabisa kutoka kwa Sheria mpaka yote yatimie.**
**[19] Yeye atakayevunja mojawapo ya amri hizi zilizo ndogo na kuwafundisha wengine kufanya hivyo ataitwa mdogo katika ufalme wa mbinguni; lakini yeyote azitendaye na kuzifunza hizi amri ataitwa mkuu katika ufalme wa minguni".**

Katika kitabu cha Matendo, tunaona viongozi wa Kikristo wa Agano Jipya wakipambana na suala hili, haswa wakati ambao watu wasio Wayahudi (watu wa Mataifa) walipokuwa Wakristo. Mwishowe walikubaliana na kiwango ambacho watu wa mataifa hawakutakiwa kuishi chini ya sheria zote za Agano la Kale. Waliandika barua kwa hawa Wakristo wapya na kuwaambia ni sheria gani za Agano la Kale ambazo wanahitaji kutii. Mjadala huu wote umeelezewa katika Matendo sura ya 15.

**Matendo 15:28-29 (Biblia Takatifu)**

**[28] Ilionekana kuwa nzuri kwa Roho Mtakatifu na kwetu kutokukubebesha na chochote zaidi ya mahitaji yafuatayo: [29] Iwe jiepushe na chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu, na damu, nyama ya wanyama walionyongwa na uzinzi. Utakuwa vizuri kuepuka mambo haya.**

Shida nyingine ya msimamo kwamba Wakristo wa leo wanatakiwa kutii sheria zote za Agano la Kale ni kwamba sheria nyingi huzungumzia kuhusu kanuni za kidini katika ibada ya hekalu, pamoja na dhabihu za wanyama. Sheria zingine zinahitaji hali ya kuvuna mazao katika miezi fulani ya mwaka, ambayo watu hawewezi kuitii katika sehemu zingine za ulimwengu ambapo msimu wa kupanda ni tofauti kabisa.

Tofauti ya msimamo huu ni kwamba Wakristo wanahitajika kutii sheria kadhaa za Agano la Kale, lakini si zote. Hii inatuweka kwa wakati mgumu wa kuamua ni sheria gani za kutii na ni zipi za kupuuza.

# Msimamo wa 2.
# Wakristo wanahitaji kutii sheria za Mungu katika Agano Jipya

Maoni mengine yaliyoshikiliwa na wengine ni kwamba Wakristo wanatakiwa kutii sheria zilizo tu katika Agano Jipya. Wanasema sheria za Agano la Kale hazihitajiki kwa Wakristo leo. Wakati Yesu alikuja duniani na kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, alitimiza sheria ya Agano la Kale, na akaanzisha uhusiano mpya kabisa wa agano na Wakristo.

1 Yohana 5:3 inasema, “Kumpenda Mungu kuna maana kwamba ni kutii Neno Lake, na Neno Lake si ngumu kulitii.” Katika Agano Jipya, Mungu ametupatia sheria nyingi zinazoeleza kile Mungu anataka tufanye na nini tusifanye. Tazama Mathayo 5, 6, na 7, Marko 12:30-31, Yohana 13:34, Warumi 13:1-2, na Waefeso 6:1-3.

### Msimamo wa 3.
### Mahali pa kuanzia kwa Wakristo wapya

Tunahitaji kuwa waangalifu sana tusije tukashikwa na malumbano juu ya sheria na tukose jambo kuu hapa. Ikiwa una nia ya dhati ya kukuza uhusiano wa kibinafsi na Yesu, basi weka vipaumbele vyako vimuangalie yeye. Hivyo ndivyo maandiko yanatwambia tufanye katika Waebrania 12:2, “Na tuelekeze macho yetu kwa Yesu.”

Yesu hatafuti tu watu watakaozitimiza sheria, Anawatafuta wale ambao wanataka kumtii kwa sababu wanampenda.

Kuzitii sheria za Mungu ni njia moja ya kuonyesha Mungu kwamba unampenda.

Watu wawili wanapooana huwa kwa matumaini wanapendana. Je, umewahi kusikia juu ya wanadoa ambao walitumia fungate yao yote wakiandika orodha kamili ya sheria zote walizopaswa kutii kwa kuwa sasa walikuwa wameoana?

Lakini ikiwa kwa kweli unampenda mumeo au mkeo, utachagua kuweka mipaka katika maisha yako, kama kielelezo cha upendo wenu mmoja kwa kila mmoja.

## C. Tii kanuni zinazoshikilia sheria za Mungu

Kuna njia nyingine ya kutatua mjadala huu mkubwa wa kuhusu ni sheria gani katika Biblia zinapaswa kutiiwa. Badala ya kujaribu kulifanya hili kuwa mjadala wa kisheria, libadilishe kuwa hali ya utaftaji wa upendo wa kweli. Ikiwa kwa kweli unampenda mtu, utataka kumpendeza mtu huyo. Ungependa kumwelewa mtu huyo, na uepuke vitu ambavyo vitamuumiza, au kuharibu uhusiano wako na yule umpendaye.

Unaweza kuchagua kuangalia kila sheria katika Biblia na ujiulize :

Je, sheria hii inaniambia nini kuhusu Mungu?

Kwa nini Mungu aliwapatia watu wake sheria hii?

Alikuwa anajaribu kuwafundisha nini kupitia kwa sheria hii?

Je, Ni somo gani au kanuni ipi ya sheria hii ambayo ninaweza kutumia kwa uhusiano wangu na Mungu leo?

Sheria katika Agano la Kale ziliandikwa kwa taifa la Israeli (Wayahudi). Walipewa zaidi ya sheria 600 ili kuwaongoza katika uoanzishaji wa serikali yao, kanuni za afya, na za kidini. Sheria hizi zilitolewa kuwasaidia katika shughuli zao za kila siku na kwa mahusiano yao ili waweze kuishi kwa maisha ya heshima na ya kumcha Mungu.

Kanuni zinazohimili kila Agano la Kale na sheria ya Agano Jipya, zinaweza kutufundisha masomo ambayo tunaweza kutumia katika hali tofauti tunazokabiliana nazo katika maisha yetu ya kila siku.

## Mafundisho ya Yesu

Hotuba ya mlimani katika Mathayo 5-7, Yesu anatoa mifano kadhaa ya jinsi ya Wayahudi wa wakati wake walikuwa wakitumia vibaya sheria za agano la kale. Kisha anafafanua jinsi Mungu anataka tuelewe sheria zake. Ufafanuzi wa Kristo unaonyesha kuwa kanuni inavyoshikilia sheria ina utenda kazi mpana zaidi ya maagizo yanayotolewa na sheria.

**Mathayo 5:21-22 Biblia Takatifu**

**“Mmesikia kwamba watu wa kale waliambiwa, ‘Usiue, na yeyote anayeua atastahili kuhukumiwa.’ Tena, mtu yeyote anayemwambia ndugu yake, ‘Raca,’ anajibika kwa Sanhedrini. Lakini mtu yeyote anayesema, ‘Mpumbavu wewe!’ atakuwa katika hatari ya moto wa jehanamu.”**

Katika sura hii, Yesu anapitia sheria moja baada ya nyingine na kupanua matumizi yake kwa kuzungumziakanuni iliyo inayoshikilia sheria hii.

## Kulisha ng’ombe na kuwalipa wahudumu

Paulo anatoa ushauri kwa Timotheo na kanisa analolichungakwa kueleza kwamba wachungaji wanapaswa kulipwa ajira nzuri. Ili kuhalalisha jambo hili, Paulo ananukuu sheria ya Agano la Kale kuhusu kulisha ng’ombe, na nukuu kutoka kwa Yesu kuhusu mishahara kwa wafanyikazi.

**1 Timotheo 5:17-18 (Biblia Takatifu)**

**17 Wazee wanaosimamia shughuli za kanisa vizuri wanastahili heshima mara mbili, haswa wale ambao kazi yao ni kuhubiri na kufundisha. 18 Maana Maandiko yanasema, “Usimfunge ng’ombe kinywa wakati wa kukanyaga nafaka,” [1] na “Mfanyakazi anastahili ujira wake.” [2]**

*Ndondoo iliyo hapo chini: 1. Kumbukumbu la Torati 25:4, 2. Luka 10:7*

Yesu na Paulo wote wanaonyesha kwa mfano kwamba sheria zote za Agano la Kale na sheria za Agano Jipya zina thamani kubwa kwa watu leo, kwa sababu kanuni zilizo zinazoshikilia kila sheria ya Mungu zinafaa kwa maswala tunayokabiliana nayo kila siku.

## Vidhibiti kasi

Biblia haitoi sheria mahususi zinazokwambia ni nini hasa cha kufanya katika kila hali unayokabiliana nayo. Kwa mfano, Biblia haina sheria inayosema, “Usiendeshe gari lakokupita kasi iliyowekwa,” au “Usitumie dawa za kulevya.” Lakini Biblia inatupatia *kanuni* ambazo tunaweza kutumia kwa kila moja ya hali hizi.

Biblia inasema katika Warumi 13:1-2 kwamba “lazima utii viongozi wa nchi.” Viongozi wa taifa letu na jimbo letu wametunga sheria zinazodhibiti mwendo wa magari. Kwa hivyo tuna jukumu la kutii mipaka hii ya kasi, kwa sababu ya kanuni iliyowekwa katika Warumi 13:1-2.

## Kuheshimu maisha

Biblia inasema katika 1 Wakorintho 6:19-20 kutoka kwa Biblia Takatifu (SUV) kwamba, mwili wako ni “nyumba ya Mungu ambamo Roho Mtakatifu anaishi…. Kwa hivyo mheshimu Mungu kwa mwili wako….” Ikiwa utatii kanuni hii ya Mungu, lazima usiharibu mwili wako kwa kutumia dawa za kulevya. Kutumia dawa za kulevya pia ni kinyume na sheria za nchi hii. Na kwa hivyo kwa njia hii pia ni makosa.

Andiko hili katika 1 Wakorintho pia linazungumzia kanuni ya kuheshimu maisha. Inatoa sababu wazi ya kutokujiua. Kanuni hii pia inachukua msimamo dhidi ya utoaji mimba.

Ni muhimu sana kwako kusoma Biblia ili kufahamu kanuni za Mungu za kuishi. Unapoanza kuiga tabia yako kulingana na kanuni hizi, utaweza kumwonyesha Mungu kwamba unampenda. Tazama Mathayo 23:23.

Roho Mtakatifu atakusaidia kuelewa kanuni zilizo nyuma ya sheria za Mungu. Pia atakusaidia kuona jinsi ya kutumia kanuni hizi kwa kila hali unayokabiliana nayo. Unapokabiliwa na shida maishani mwako, jiulize, “Ni maandiko gani katika Biblia yanayotoa mwongozo wa jinsi ya kujibu kwa njia ambayo itampendeza Mungu?”

# D. “Mapenzi ya Mungu” ni nini?

Tumeangalia jinsi ninaweza kuonyesha Mungu kwamba ninampenda kwa kutii sheria zake, na kutii kanuni zinazohusu sheria hizo. Njia nyingine ambayo ninaweza kuonyesha Mungu kwamba ninampenda ni kwa kumpa haki zangu za kibinafsi. Tazama *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya,* **Hasira na Haki za Binafsi** kwa habari zaidi juu ya mada hii.

Sasa natuangalie njia nyingine ambayo tunaweza kumonyesha Mungu tunampenda. Ninaweza kuonyesha Mungu ninampenda kwa kufanya kile Anachotaka nifanye. Mara nyingi hili linajulikana kama- “kufanya mapenzi ya Mungu.” Hii inamaanisha nini? — ni kufanya kile Mungu anataka nifanye kama vile anavyokiweka wazi kwangu.

Tutaangalia mambo mbali mbali ambayo Mungu anataka uanze kufanya hivi sasa — leo!

Mungu ana mpango kwa maisha yako, na ni mpango mzuri

1. Kuwa Mkristo
   Warumi 10:9
   2 Petro 3:9
2. Acha kutenda dhambi
   1 Petro 2:11
   1 Wathesalonike 5:22
3. Anza kufanya mamabo yaliyo sawa
   Warumi 12:1,2,9
4. Jitolee kufanya huduma ya Kikristo
   Mathayo 6:19-21
5. Kabiliana na shida na ujaribu kwa njia ambayo Mungu anataka utende
   Yakobo 1:2-4

6. Jifunze kujibu kama vile Mungu anavyofanya
   Warumi 8:29
7. Jifunze kujali mahitaji ya wengine
   1 Wakorintho 13:4-8
8. Waambie wengine yale ambayo Kristo amekufanyia
   1 Petro 3:15

Unaweza kuanza kufanya haya yote sasa hivi. Hivi ndivyo Mungu anataka ufanye. Hauhitaji kusubiri hadi upokee ishara maalum kutoka mbinguni kabla ya kufanya mambo haya.

Lakini kuna maamuzi mengine ambayo utakabiliana nayo maishani mwako ambapo utataka kuwa na uthibitisho wazi kwamba hili ndilo Mungu anataka ufanye. Katika visa hivyo, unaweza kutafuta mwongozo wa Mungu kwa kusoma Biblia, kusali, na kutafuta ushauri wa watu wanaomcha Mungu.

## Ushawishi wangu binafsi kutoka kwa Mungu

Ushawishiwa wa kibinafsi ni mpaka wa kibinafsi kutoka kwa Mungu kukusaidia na kukukinga. Roho Mtakatifu mara nyingi hushughulika na watu kuhusu mambo fulani ambayo Yeye hataki wafanye. Kwa mfano, watu wengine wana imani za kibinafsi juu ya kunywa divai, kwenda kwenye sinema, aina fulani ya mavazi, au jinsi ya kutumia pesa zao. Hukumu hizi za kibinafsi ni sehemu muhimu ya mapenzi ya Mungu kwa mtu huyo.

Njia nyingine ya kueleza jambo hili itakuwa “sheria ya kibinafsi,” au “mpaka wa kibinafsi” ambao Mungu amekupa ambao si lazima uwe sheria ya kibiblia ambayo Mungu ametoa kwa ulimwengu wote kutii. Unaweza kuwa na hakika kwamba ushawishi wote wa kibinafsi kutoka kwa Mungu ni mpaka wako mkali kuliko sheria zilizotajwa katika Biblia.

Mungu hatakupa dhamira ya kibinafsi kwamba ni sawa kufanya ngono nje ya ndoa, maadamu unampenda mtu huyo. Hiyo itakuwa kinyume kabisa na yale ambayo Mungu ameyasema katika Biblia.

Kwa kila ushawishi wa kibinafsi kutoka kwa Mungu, tunahitaji kuuangalia kwa njia ile ile tunayoangalia kila sheria ya Mungu - ni kanuni gani ya kukubalika iliyo nyuma ya ushawishi huu na inayonisaidia kuelewa Mungu na ni kwa nini anataka nijibu kwa njia hii?

Tunachozungumza hapa ni ushwawishi wa kibinafsi ambao Mungu amemwongoza mtu afanye. Hatuzungumzii masilahi ya kibinafsi ambayo mtu amechagua mwenyewe.

## Masilahi ya kibinafsi

Kikundi kingine cha chaguo ni pamoja na chaguo za kibinafsi ambazo watu hufanya kuhusu mitindo yao ya maisha. Kwa mfano, watu wengine hawapendi kuvaa nguo za kahawia. Chaguo lao la kibinafsi ni kuvaa nguo za rangi zingine. Hivyo ni sawa - lakini hilo ni chaguo la kibinafsi, si ushawishi ambao Mungu ameweka kwa mtu huyo.

Watu wengine huchagua kutokula vyakula fulani. Huenda daktari aliwaambia wazuie kula vyakula fulani kwa ajili ya ubora wa afya yao. Kuweka mpaka huo wa kibinafsi maishani mwako wa kufuata ushauri wa daktari kwa hakika ni jibu la busara. Lakini huu si lazima uwe ushawishi wa kibinafsi kutoka kwa Mungu.

## Shawishi za Kibinafsi za watu wengine

Tunahitaji kwa uangalifu kuheshimu imani za kibinafsi za watu wengine.

**Warumi 14:20-22 (Biblia Takatifu)**

**Usibomoe kazi ya Mungu juu ya kile unachokula. Kumbuka, hakuna kitu kibaya na vitu hivi vyenyewe. Lakini ni vibaya kula chochote ikiwa kinamfanya mtu mwingine ajikwae. 21Usile nyama au usinywe divai au usifanye kitu kingine chochote ikiwa kinaweza kumsababisha Mkristo mwingine kujikwaa. 22Unaweza kuwa na imani ya kuamini kuwa hakuna kitu kibaya kwa kile unachofanya, lakini kiweke kati yako na Mungu. Heri wale ambao hawajihukumu kwa kufanya jambo ambalo wanajua ni sawa.**

Wakati huo huo lazima pia tuwe waangalifu kwamba hatulazimishi imani zetu za kibinafsi kwa wengine. Kwa sababu tu Mungu anataka uwe na ushawishi wa kibinafsi haimaanishi kila mtu mwingine anapaswa kufuata mfano wako.

Suala halisi hapa ni-je, unampenda Mungu sana hivi kwamba unataka kumtii kwa kila eneo la maisha yako? Viwango vya kibinafsi unavyojiwekea vinaweza kukusaidia kuinua tabia yako - kuwa kama Yesu kila siku.

Tazama pia 1 Petro 2:16 na angalia jinsi mapenzi ya Mungu yanahusiana na sheria za Mungu.

Wewe hukabiliwa na maamuzi makubwa na madogo maishani mwako. Mungu anataka uone umuhimu wa kutafuta mwongozo wake. Mungu ana mpango kwa maisha yako, na ni mpango mzuri. Iwe ni kuchagua kazi yako, au kuamua kuoa au kubaki bila kuoa au kuolewa- Mungu ana mpango na wewe.

**Yeremia 29:11 (Bibilia Takatifu)**

**"Kwa maana najua mipango niliyonayo juu yenu," asema BWANA, "nina mpango wa kufanikiwa na sio kukudhuru, mipango ya kukupa tumaini na wakati ujao."**

**Waefeso 2:10 (Biblia Takatifu)**

**Kwa maana sisi ni kazi ya Mungu, iliyoundwa katika Kristo Yesu kufanya matendo mema, ambayo Mungu aliandaa mapema ili tufanye.**

Unaweza kumpuuza Mungu, au unaweza kusema, "Mungu nataka kufanya kile Unachotaka nifanye. Nisaidie kuona kile Unachotaka nifanye." Yesu alionyesha kujitolea kwake kufuata mpango wa Mungu kwa maisha yake.

**Yohana 5:19-20 (Biblia Takatifu)**

**Yesu akawajibu, "Kweli nawaambieni, Mwana hawezi kufanya kitu peke yake; anaweza tu kufanya kile anachomwona Baba yake akifanya, kwa sababu kila Baba anachofanya Mwana pia hufanya. Kwa maana Baba anampenda Mwana na anamwonyesha yote anayofanya."**

Tunaweza kufuata mfano wa Yesu na kuyafanya malengo yetu ya kila siku yawe ni ya kufanya kile ambacho Mungu anataka tufanye. Kadiri unavyofanya hili kuwa sehemu ya maamuzi yako ya kila siku, ndivyo utajifunza zaidi jinsi ya kufanya hivyo.

# Sura ya 4
# Matokeo ya kumtii Mungu

Ni nini hutokea ninapotii sheria za Mungu? Mara nyingi sisi hukosa athari za matendo yetu — hatutambui athari kubwa ya matendo yetu ya utii na jinsi yanavyowaathiri wengine.

Wakati Musa aliwaongoza Wayahudi kutoka Misri na kuwaandaa kwa ajili ya kuingia kwa nchi yao mpya ya ahadi, aliwawasilishia ujumbe wazi kabisa kutoka kwa Mungu.

**Kumbukumbu la Torati 11:26-28 (Biblia Takatifu)**

**26 Tazama, ninaweka mbele yako leo baraka na laana- 27 baraka ukitii amri za Bwana, Mungu wako, ninazokupa leo; 28 laana ikiwa utayaasi maagizo ya BWANA, Mungu wako, na kuiacha njia nikuagizayo leo, kwa kufuata miungu mingine, ambayo wewe huijui.**

Mungu alisema wazi kwamba ikiwa wangemtii, wangepata baraka Yake maishani mwao. Vivyo hivyo jambo hili ni kweli kwetu leo — ikiwa tutatii sheria za Mungu, tunaweza kuwa na hakika kwamba baraka Yake itakuwa katika maisha yetu.

Kumtii Mungu hakufanyi upokee wokovu — tiketi yako ya kwenda mbinguni. Wokovu ni kipawa cha thamani kutoka kwa Mungu. Kama onyesho la upendo wako kwa Mungu, utii wako hudhihirisha kuwa unataka kuishi kwa uhusiano mwema na Yeye. Sisi sote tunahitaji mipaka yake ili atulinda kutokana na mambo ya uharibifu ambayo yanaweza kuharibu maisha yetu.

Njia nyingine ya kuangalia matokeo ya utii ni kujibu swali hili:

Je, utii kwa Mungu unaathiri vipi mahusiano yangu na watu hawa?

1. Mungu
2. Mimi mwenyewe
3. Wazazi wangu na familia
4. Wanangu
5. Marafiki zangu
6. Wale ninaofanya nao kazi
7. Watu wengine, pamoja na watu ambao hata sijui

Jinsi unavyochagua kumtii Mungu hakuathiri tu uhusiano wako na Mungu, bali pia kunaathiri uhusiano wako na watu wengi ambao wako karibu nawe.

## Yusufu akabiliwa na uchaguzi mgumu

Akiwa kijana, Yusufu aliuzwa na ndugu zake, na akamalizia kuishi kama mtumwa kule Misri katika nyumba ya Potifa. Hapo awali tunaona matokeo ya kumtii Mungu.

**Mwanzo 39:2-4 (Biblia Takatifu)**

**Bwana alikuwa pamoja na Yusufu na alifanikiwa, na aliishi katika nyumba ya bwana wake Mmisri. [3] Bwana wake alipoona ya kuwa BWANA yu pamoja naye, na ya kuwa Bwana amemfanikisha katika yote aliyoyafanya, [4] Yusufu akapata kibali machoni pake, akamtumikia. Potifa alimfanya awe msimamizi wa nyumba yake, naye akamkabidhi kila kitu alichokuwa nacho.**

Baada ya muda fulani, mke wa Potifa alijaribu kumtongoza Yusufu. Yusufu alikabiliwa na uchaguzi mgumu — iwapo aamue kumtii Mungu, au amkasirisha mke wa Potifa.

**Mwanzo 39:6-9 (Biblia takatifu)**

**Basi Yusufu alikuwa na afya njema na kupendeza, [7] na baada ya muda mke wa bwana wake alimtambua Yusufu, akasema, "Njoo ulale nami." [8] Lakini yeye alikataa.... [9] "Je, nitafanyaje uovu kama huu na kumtendea Mungu dhambi?"**

Kwa hivyo Yusufu alichagua kutii Mungu, na baadaye akakabiliwa na shida kubwa. Mke wa Potifa alimshtaki kwa ubakaji na Yusufu akajikuta gerezani.

Kuna wakati ambapo kumtii Mungu kunakuweka kwa shida kubwa. Lakini unaweza kuwa na hakika kwamba kama vile Mungu alikuwa na Yusufu katika kila hali, Mungu atakusaidia kukabiliana na kila shida inayokujia kama matokeo ya kumtii Yeye.

## Shadraki, Meshaki, na Abednego

Katika kitabu cha Danieli sura ya tatu tunapata hadithi ya vijana watatu ambao pia waliwekwa katika hali ngumu walipochagua kumtii Mungu. Chaguzi zao sahihi zinawaweka katika hali ngumu iliyokuwa na matokeo ya kuishi-au-kifa. Waliamriwa kuinama na kuabudu sanamu mpya ya mfalme Nebukaneza.

Walipokataa kuabudu sanamu hii, waliletwa mbele ya mfalme. Aliwapa chaguo, la kuinama na kuabudu sanamu hii au watupwe katika tanuru ya moto. Mungu kimiujiza aliwaokoa dhidi ya kujeruhiwa kwa Shadraki, Meshaki, na Abednego, na wakatoka ndani ya tanuru wakiwa hai. Mfalme na taifa zima waliathiriwa na tendo hili la utii.

Hali nyingi unazokabiliana nazo kila siku si za kushangaza kama vile wanaume hawa watatu walikabiliwa nayo siku hiyo. Haijalshi swala hilo ni kubwa au ndogo kiasi gani, chaguo lako la kumtii Mungu lina athari kubwa kwako na kwa watu waliokaribu nawe.

## Kitendo cha utii cha Brian

Brian aliendeleza tabia yake ya dawa za kulevya kwa kuiba kutoka kwa wengine. Baada ya kujiunga na Teen Challenge na kuacha maisha yake ya zamani, na akajifunza kuhusu maana ya kuwa na uhusiano wa kibinafsi na Yesu. Miezi kadhaa baadaye alipokuwa akiomba na kusoma Biblia, alihisi Mungu akisema na moyo wake kwama arudisha pesa alizokuwa ameiba kutoka kwa benki.

Alihitimu kutoka kwa Teen Challenge na kupata kazi, na akaanza kuweka akiba ya pesa ili kulipia kile alichokuwa ameiba. Alijaribiwa kuweka tu pesa kwenye bahasha ambayo haikuwa imeandikwa jina na kuipeleka kwa benki ikiwa na maneno – hamna sahihi. Lakini moyoni mwake, alihisi Bwana akimshawishi, kwamba hapaswi kutumia mkakati huo.

Mwishowe alihifadhi pesa na kumpigia simu rais wa benki ili kuwa na miadi ya kurudisha pesa zile. Katibu wa banki aliandika chini miadi hiyo, lakini akapiga simu tena kumwambia kwamba benki italazimika kuripoti kwa polisi kile alikuwa akipanga kufanya. Hii ilimweka Brian katika hali gumu kwa sababu alikuwa kwa uchunguzi mwingine tayari kwa shtaka lingine. Ikiwa polisi wangefuatilia matendo yake, angefungwa gerezani kwa sababu ya kumtii Mungu.

Siku aliyokutana na msimamizi wa benki wakati wa kirudisha pesa, alikumbana na mambo kadhaa ambayo hayakutarajiwa - kwanza msimamizi wa benki alitaka kujua ni kwa nini alikuwa akirudisha pesa hizo. Ikawa nafasi nzuri kwa Brian kumweleza juu ya mabadiliko ambayo Yesu alikuwa amefanya katika maisha yake. Mazungumzo yakaendelea kwa dakika 45.

Walipoondoka kwenye ofisi ya msimazi wa benki, Brian alisema, “Ilionekana kama uzito wa pauni 400 uliondolewa mabegani mwangu!” Katika siku na miaka iliyofuata Brian angeweza kuangalia nyuma juu ya faida ambazo alipokea kama matokeo ya kumtii Mungu — hakukuwa na majuto, hakuwa na hofu, ilikuwa ni amani ya Mungu tu.

Lakini kitendo cha utii cha Brian kiliathiri watu wengi zaidi kuliko vile alivyotarajia. Kitendo hiki kilikuwa na athari kubwa kwa msimamizi wa benki kuliko vile alivyotarajia. Na Mungu anajua tu ni watu wangapi msimamizi huyu wa benki aliwaambia juu ya matendo ya Brian. Na watu ambao Brian hajawahi kukutana nao wamesikia kuhusu kitendo chake cha utii na wakapata ujasiri pia kumtii Mungu.

Biblia na mifano ya kila siku leo hii kama vile ya Brian inazungumzia kuhusu matokeo ya utii. Hapa kuna maandiko ambayo yanaeleza baadhi ya matokeo ya utii.

1. Kutoka 19:3-6
2. Kumbukumbu la Torati 11:26-28
3. Ayubu 36:11
4. Mithali 2:21
5. Yeremia 7:23
6. Malaki 3:7-12
7. Yohana 14:15-16
8. Yohana 14:21, 23
9. Yohana 15:10,11
10. Warumi 5:18-19
11. Warumi 6:16
12. Warumi 6:23
13. Warumi 13:1-6
14. Waefeso 6:1-3
15. Waebrania 5:8-9
16. 1 Petro 2:13-17

Njia nyingine unayoweza kuanza kuona matokeo ya kumtii Mungu ni kuandika yale unayoyapitia katika maisha yako ya kila siku na mahali ambapo ulikuwa na chaguo la kumtii Mungu. Ni nini kilifanyika? I Huenda hadithi yako isiwe ya kustaajabisha kama ile Brian alipitia.

Mara nyingi chaguzi ndogo zinaonekana kuwa na athari kidogo au hazina athari yoyote katika maisha yetu. Lakini zinatuandaa kwa changamoto kubwa zaidi ambazo tutakabiliana nazo katika siku zijazo. Kwa hivyo kwa kweli, vitendo hivi vidogo vya utii vina athari kubwa katika maisha yetu wakati vinapoonekana kwa muda mrefu.

**Luka 16:10 (Biblia Takatifu)**

**Yeyote anayeweza kuaminiwa na kidogo sana pia anaweza kuaminiwa na mengi, na yeyote ambaye ni mwaminifu kwa kidogo sana atakuwa mwaminifu kwa mengi.**

# Sura ya 5
# Matokeo ya kutomtii Mungu

Ni nini hutokea ninapokosa kutii? Shetani anataka uamini kuwa hakuna chochote kibaya kitakutokea wewe au mtu mwingine yeyote yule ikiwa utakiuka sheria za Mungu. Hata hivyo hili si kweli. Biblia inafundisha wazi kwamba ni makosa kutomtii Mungu.

Biblia hutumia neno rahisi la herufi 6 kuelezea uasi wote - DHAMBI. Mungu anaahidi kwamba dhambi zote zitaadhibiwa. Huenda adhabu isije mara moja, lakini lazima itakuja.

## A. Ninaweza kujifunza nini kutokana na kutotii kwa wengine?

Mungu ametoa picha ya kweli kabisa ya watu katika Biblia. Hatusomi tu mafanikio yao, tunaona pia kushindwa kwao na dhambi zao pia. Biblia inasema matukio haya yaliwekwa katika Biblia ili kuwa mifano kwetu - kwa hivyo tunaweza kujifunza kutoka kwa makosa yao, na si kufanya makosa sawia na hayo katika maisha yetu ya kila siku.

Kile Mungu aliwaambia Wayahudi miaka elfu kadhaa iliyopita bado ni kweli leo hii.

**Kumbukumbu la Torati 11:26-28 (Biblia Takatifu)**

**26 Tazama, ninaweka mbele yako leo baraka na laana- 27 baraka ukitii amri za Bwana, Mungu wako, ninazokupa leo; 28 laana ikiwa utayaasi maagizo ya BWANA, Mungu wako, na kuiacha njia nikuagizayo leo, kwa kufuata miungu mingine, ambayo wewe huijui.**

### Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni

Matendo yote ya kutotii huwa na matokeo yake. Adamu na Hawa walijifunza hii mapema katika Bustani ya Edeni. Shetani aliibua swali, “Je, kweli Mungu alisema, ‘Usile kutoka kwa mti wowote katika bustani’?” Mwanzo 3:1

Hawa alijibu kwa kutumia maagizo ya Mungu, akisema kwamba ikiwa watakula matunda kutoka kwa mti katikati ya bustani, watakufa. (vs. 2-3)

Hawa kisha akaanguka kwa mtego ambao Shetani aliutumia vyema, ambao unatumika vyema leo hii -aliamini uongo wake.

**Mwanzo 3:4-5 (Biblia Takatifu)**

**“Hakika hautakufa,” nyoka akamwambia mwanamke. 5 “Kwa maana Mungu anajua kwamba mtakapokula matunda yake, macho yenu yatafunguliwa, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.”**

Badala ya kumtii Mungu, alichagua kumwamini Shetani na akafurahia kula tunda lililokatazwa. Raha hiyo ilidumu kwa dakika chache, na Adam alifanya vivyo hivyo. Lakini kitendo hiki kimoja cha kutotii kulianzisha mfuatano mrefu wa matokeo mabaya. Tendo kama hilo "dogo" la kutotii lilibadilisha ulimwengu wote, na kuleta laana ya dhambi kati ya maisha yake na ulimwenguni kote. Leo bado tunateseka kwa sababu ya matokeo ya kutotii kwake.

## Mfalme Daudi na Bathsheba

Katika kitabu 2 Samweli 11-12 tunapata hadithi ya Mfalme Daudi na kitendo chake cha kutotii, na safu mbaya ya matukio yaliyofuata dhambi yake. Lilianza kama tendo moja la mapenzi-alimuona mwanamke akioga na akatumana aletwe kwake. Alipokuja, alilala naye, ingawa alijua alikuwa ameolewa na mmoja wa viongozi wake wakuu wa jeshi. Alipuuza kile Mungu alisema katika amri 10 – amri ya 7 – "Usizini." Kutoka 20:14 Biblia Takatifu (SUV)

Pindi Mfalme Daudi alinaswa na mfululizo wa matokeo kadhaa ambayo yote yalishikamanshwa na wakati wake mfupi wa raha na Bathsheba. Haikuchukua muda mrefu ambapo Bathsheba alimletea Daudi ripoti kwamba alikuwa mjamzito. Mfalme anamwita mumewe Bathsheba kutoka vitani na kumwagiza ajiunge na mkewe nyumbani kama njia yake Daudi ya kuficha dhambi yake.

Lakini Uria anachagua jibu la heshima na kusema la, na analala kwenye kasri pamoja na walinzi kwani wanajeshi wenzake wote bado walikuwa vitani.

Jaribio la Daudi la kuficha dhambi yake linakosa kufua dafu, anaingia katika dhambi zaidi. Anapanga njama za kumuua Uria, kwa kuwafanya majenerali waaminifu wa jeshi lake kumsaliti Uria mikononi mwa adui, na kusababisha kifo cha Uria. Kwa kila uamuzi usiofaa uliofanywa na Daudi, watu zaidi wanaathiriwa na dhambi yake.

Baada ya kifo cha Uria, Daudi anaoa Bathsheba, na mtoto anazaliwa. Lakini Mungu hakufurahishwa na hilo, hivyo akamtuma nabii Nathani kumkabili Daudi kutokana na dhambi zake. Mtoto huyo alikufa baada ya siku chache. Daudi anakubali dhambi hizo, lakini bado anakabiliwa na athari, ambazo zinamuathiri kwa maisha yake yote.

Na la kusikitisha ni kwamba, watu leo bado wanatumia dhambi ya Daudi na Bathsheba kuhalalisha kushindwa kwao kumtii Mungu.

Kuna mifano mingi zaidi katika Biblia ya matokeo ya kutomtii Mungu. Kila mmoja hutoa mfano mzuri wa jinsi hatupaswi kufuata hatua zao, au sisi pia tutapata matokeo mabaya ya dhambi.

Suala moja zaidi – hakuna kitu kama dhambi "salama". Kondomu inaweza kupunguza hatari ya mtu kuambukizwa ugonjwa fulani, lakini kuna matokeo mengine kando na magonjwa ya mwili. Kila tendo moja la kutotii linatufungulia matokeo mabaya.

# B. Maneno manne muhimu yanayohusiana na kutotii

Tunapoangalia kwa karibu kile kinachotokea katika maisha yetu tunapomwasi Mungu, kuna maswala manne ambayo tunahitaji kuelewa. Maswala haya manne ni – matokeo ya asili, nidhamu, adhabu, na kulipiza kisasi – mara nyingi maeno haya hueleweka vibaya, haswa kwa uhusiano wake na matendo yetu ya kutomtii Mungu.

## 1. Matokeo ya asili

Tunapomwasi Mungu, kila wakati kuna matokeo. Hizi si sawa na nidhamu au adhabu.

Mzazi anamwambia mtoto "Usiguse jiko. Ni moto." Ikiwa mtoto hatatii na kugusa jiko, matokeo ya asili ya kitendo hicho cha kutotii ni mtoto atachomeka kidole chake.

Daktari wa matibabu kwa jina S. I. McMillen katika kitabu chake, **None of These Diseases,** alizungumzia kuhusu baadhi ya matokeo ya asili ya kutii au kutotii baadhi ya sheria za afya za Mungu. Unaweza kusoma kitabu hicho na uone jinsi sayansi ya matibabu ya kisasa imethibitisha matokeo haya mabaya ya kutotii sheria za Mungu.

Matokeo ya asili ni hayo tu - yani matokeo ya asili ya kufanya jambo fulani. Matokeo haya si sawa na nidhamu au adhabu. Tunapomwasi Mungu, huenda tusione matokeo mara moja, lakini wakati matokeo haya yatakuwa wazi zaidi.

**Wagalatia 6:7-10 (Biblia Takatifu)**

**Usidanganyike: Mungu hawezi kubezwa. Mtu huvuna alichopanda. 8 Yeye apandaye ili apendeze tabia yake ya dhambi, kutokana na maumbile hayo atavuna uharibifu; yeye apandaye ili kumpendeza Roho, kutoka kwa Roho atavuna uzima wa milele. 9Tusichoke katika kutenda mema, kwa kuwa kwa wakati ufaao tutavuna ikiwa hatutakata tamaa. 10Kwa hiyo, tukiwa na nafasi, na tuwatendee watu wote mema, haswa wale wa jamaa ya waumini.**

Wakati mwingine tunapofushwa na matokeo haya, lakini watu wengine walio karibu nasi wanaweza kuona uharibifu. Ikiwa hauoni atahri ya kutomtii Mungu, unaweza kujadili hii na Mkristo aliyekomaa zaidi na upate ushauri wao.

Unaweza pia kujifunza kuona matokeo haya unaposoma hadithi kwenye Biblia ya kutotii kwa wengine. Angalia hasa kwa kile kilichotokea katika maisha yao kama matokeo ya dhambi zao.

Tunaweza kuangalia matokeo ya kutomtii Mungu kwa kujibu swali hili:
Je, kutomtii Mungu kunaathiri vipi uhusiano wangu na watu hawa?

1. Mungu
2. Mimi mwenyewe
3. Wazazi wangu na familia
4. Watoto wangu (wa sasa au wa baadaye)
5. Marafiki zangu
6. Watu wengine, pamoja na watu ambao hata sijui.

Matokeo ya kutotii ni mabaya zaidi kuliko yale tunayotarajia. Kwa kweli, wengi wetu huwa tunajibu kama Hawa, tunaangalia jaribu na kupuuza kile Mungu amesema, na kuangalia raha ya wakati mfupi. Shetani huwa haweki ishara ya tahadhari kuhusu matokeo ya dhambi zetu. Yeye kimsingi hufanya tuzingatie furaha ya muda.

Wakati mzuri wa kuzingatia matokeo ya kutomtii Mungu ni kabla ya kutenda. Hili haliji ukawaida. Utalazimika kujizoeza kuuliza swali hili kabla ya kuchukua hatua - matokeo yatakuwa nini ikiwa nitachagua kufanya hivi? Kwa kweli inaweza kukuokoa kutokana na huzuni nyingi na shida ikiwa itakusaidia kuchagua kumtii Mungu kuliko kutomtii.

## 2. Nidhamu

Tunapomwasi Mungu, mara nyingi yeye hutuadhibu. Nidhamu hubeba wazo la kurekebisha shida. Lengo la nidhamu ni kumsaidia mtu kuishi akiwa sawa - kuchagua kutii wakati huo mwingine anapokabiliwa na chaguo jingine.

Waebrania 12:5-13 inaeleza ni kwa nini Mungu anatuadhibu. Walakini, unahitaji kujua kwamba tafsiri zingine za Biblia hutumia neno "kuadhibu" hapa badala ya nidhamu. Katika visa hivi, mtafsiri hatoi tofauti finyu iliyoko kati ya adhabu na nidhamu ambayo tunafanya hapa katika somo hili. Katika visa vingi katika Biblia, neno "adhabu" limetumika kwa maana pana sana kujumuisha aina yoyote ya nidhamu au marekebisho.

**Waebrania 12:10-11 (Biblia Takatifu)**

**Baba zetu walituadhibu kwa muda kidogo kama walivyofikiria; lakini Mungu hutuadhibu kwa faida yetu, ili tushiriki utakatifu wake. 11 Hakuna nidhamu inayoonekana kuwa ya kupendeza wakati huo, lakini yenye kuumiza. Baadaye, hata hivyo, huzaa mavuno ya haki na amani kwa wale ambao wamefundishwa nayo.**

Mungu hutuadhibu kwa sababu anatupenda, na anataka kile kilicho kizuri kwaajili yetu. Kila moja ya sheria za Mungu zimetengezwa kutulinda kutokana na vitu vinavyoharibu na kuathiri maisha yetu.

Nidhamu hubeba kipengele cha tumaini. Nidhamu hiyo hutolewa na matumaini kwamba itasababisha mabadiliko mazuri katika maisha ya mtu asiye mtiifu. Aina yoyote ya nidhamu anayotumia Mungu maishani mwako ina uwezo wa kukupa ufahamu mzuri wa njia sahihi ya kuishi.

Mfano mmoja wa nidhamu ni kushauri mtu afanye kazi tena, wakati huu kwa njia sahihi. Kwa mfano, hebu tuseme una wakati mgumu sana kuelewana na mtu ambaye ana mtazamo fulani ambao unakukera sana. Kila wakati unapokuwa karibu na mtu huyu, unajikuta ukijibu kwa njia isiyo ya fadhili kama vile Yesu angefanya. Badala yake unaona ni rahisi kubishana na mtu huyo na kumkasirikia.

Mungu anataka ujifunze jinsi ya kumpenda mtu huyo. "Wapende?" unajibu, "Laiti wangeondoka kwenye maisha yangu! Nitafurahi sana, ikiwa kamwe sitawaona tena. Kwa kweli, uwepo wao maishani mwangu ni mojawapo ya sababu kuu ya masumbufu mengi kwa siku zangu. Ningeweza kufurahia kila siku isingekuwa mtu huyu!"

Nidhamu ya Mungu inaweza kuendelea kuleta aina hii ya “watu wanaokukera” maishani hadi ujifunze jinsi ya kuwajibu kwa njia njema na ya upendo. Badala ya kuwalaumu kwa mitazamo yao mibaya, unahitaji kujifunza jinsi ya kuwajibika kwa mitazamo na majibu yako mwenyewe.

Mungu anataka urekebishe tabia na mitazamo yako hata kama mtu huyo habadiliki.

## 3. Adhabu

Adhabu, kama tunavyoifafanua hapa, inabeba dhana kwamba aina fulani ya uzoefu mchungu unawekwa juu ya mtu asiye mtiifu ili kumwadhibu kwa matendo yake ya kutotii. Adhabu hubeba wazo kwamba mtu asiye mtiifu anapaswa kuteseka kwa matendo yake.

Adhabu haina lengo lake la kwanza la kusaidia kurekebisha shida, ila inazingatia kumfanya mtu alipe adhabu kwa tabia yake ya kutotii.

Lengo la muda mrefu la adhabu ni kuleta mabadilko ya tabia. Lakini njia iliyochukuliwa kufikia hali hiyo huanza kwa adhabu iliyo na machungu. “Tunatumai maumivu ya adhabu yatakuchochea ubadilike,” ndiyo hoja inayosababisha adhabu.

Mungu mara nyingi atatumia nidhamu kama jibu lake la kwanza kutufanya tutii. Walakini, wengine wetu ni wagumu sana wa kusikiliza marekebisho Yake. Kwa hivyo Mungu mara nyingi hutumia adhabu kutufanya tuone jinsi alivyo makini ili kwamba tubadilike.

Unapoangalia tena dhambi ya Mfalme Daudi na Bathsheba katika kitabu cha 2 Samweli 11-12, adhabu ya Mungu ilikuwa kuchukua uhai wa mtoto aliyezaliwa. Hili halikuwa tokeo lolote ambalo mtoto alifanya, lakini ilikuwa ni dhambi ya Daudi ambayo ilikuwa ikiadhibiwa. Unaweza kusema, “Hiyo ni adhabu kali mno.” Lakini Mungu daima ni mwadilifu katika nidhamu na adhabu yake.

Watu wengine wanamtazamo mbaya juu ya jinsi Mungu anavyotuadhibu. Wanaangalia kila shida inatokea katika maisha yao kama kielelezo cha hasira ya Mungu dhidi yao. Kwa mfano, kila wakati wanajikwaa kidole, au kuvunja glasi, au kupata tairi lililopasuka-wanazitafsiri kama adhabu ya Mungu.

Kuna nyakati ambapo Mungu hutumia mazingira katika maisha yetu kama njia ya kutuadhibu. Lakini kila jambo “baya” linalotokea siku nzima halipaswi kutafsiriwa kama adhabu kutoka kwa Mungu. Mungu haangalii njia za kijanja za kulipiza kisasi kwa watu wasio watiifu.

Agano la Kale lina mifano kadhaa ya njia tofauti ambazo Mungu aliwaadhibu watu wasiotii. Wakati mwingine alizuia mvua, akatuma mapigo ya wadudu, na mambo mengine sawia na hayo maishani kama njia ya kuwasaidia watu kuoana dhambi, waikubali na warejelee hali ya kumfuata.

## 4. Kisasi

Kulipiza kisasi ni tofauti kabisa na maswala mengine matatu ambayo tumeangalia hapo awali. Kulipiza kisasi kunalenga kumlipa yule aliyekosea. Ikiwa Jim alimpiga kaka yako mdogo, basi utampiga Jim au kaka yake mdogo.

Kulipiza kisasi ni kujichukulia kwa mikono yako mwenyewe jukumu la kumwadhibu mtu aliyefanya kosa.

Kulipiza kisasi kunapuuza mahusiano ya mamlaka na majukumu ambayo viongozi wanayo ya kuona kwamba nidhamu inayofaa inatolewa kwa mtu ambaye hajatii. Warumi 12:17-21 inatuambia kile Mkristo anapaswa kufanya kuhusu kulipiza kisasi. Mungu anasema, “Niachie kisasi.”

**Warumi 12:19 (Biblia Takatifu)**

**Usilipize kisasi, marafiki zangu, bali wacha nafasi ya ghadhabu ya Mungu, maana imeandikwa: “Ni yangu kulipiza kisasi; Nitalipa,” asema Bwana.**

Mafundisho ya Biblia yanaweka wazi kuwa tunapaswa kujibu kwa fadhili na upendo kwa wale ambao hawaitii. Achia viongozi wako na Mungu maswala ya nidhamu na adhabu.

Si kila mtu asiye mtiifu ambaye huadhibiwa mara moja kutokana na matendo yao mabaya. Lakini Neno la Mungu linaweka wazi kuwa kila mtu atakabiliana na Mungu mwishoni mwa maisha yake ili kutoa hesabu ya matendo yake yote. Hukumu ya haki inawezakana isije wakati wa maisha yao, lakini hakuna mtu atakayeepuka haki ya Mungu watakapokufa.

Biblia imejaa mifano mibaya ya matokeo ya kutotii. Hapa kuna maandiko machache ambayo yanazungumza juu ya matokeo ya kutotii. Unapoangalia kila moja ya mifano hii, angalia matokeo ya matendo yao. Je, Mungu aliwaadhibu vipi? Je, Aliwaadhibu — vipi? Je, Watu waliohusika walitafuta kulipiza kisasi na kutoa adhabu yao wenyewe kwa vitendo vya uasi vya mtu huyo?

1. Kumbukumbu la Torati 11:26-28
2. 1 Samweli 13 na 14
3. 2 Samweli 11 na 12
4. Ayubu 36:12
5. Mithali 2:22
6. Mithali 5:22-23
7. Mithali 6:29
8. Mithali 13:13
9. Mithali 15:9-10
10. Yeremia 12:17
11. Malaki 3:7-12
12. Warumi 5:18-19
13. Warumi 6:16
14. Warumi 6:23
15. Warumi 13:1-6
16. 1 Petro 2:13-17

# C. Je, Mtazamo wa Mungu ni nini kwa watu wasiotii sheria zake?

Watu wengine wanafikiri kwamba Mungu ana hasira juu yao kila wakati wanapokaidi sheria zake. Wanaamini kuwa anawasubiri waondoke kwenye mapenzi yake ili awaadhibu.

Wengine hupuuza Mungu kabisa na hawafikirii kamwe jinsi Mungu anahisi kuhusu matendo yao.

Wakati mtu anakuwa Mkristo, mara nyingi huwa na wasiwasi mkubwa jinsi Mungu anahisi kuwahusu. Biblia iko wazi kwa kusema kwamba Mungu anampenda kila mmoja wetu - hata wakati tulikuwa bado tunaishi katika dhambi, tukiwa mbali naye.

Kwa hivyo ni nini mtazamo wa Mungu kwa watu wasiotii sheria zake?

## 1. Mungu huhuzunika tunapotenda dhambi

Zaidi ya yote, Mungu huwa na huzuni tunapotenda dhambi. Wakati Yesu alilia juu ya Yerusalemu, alionyesha upendo na huzuni aliyokuwa nayo kwa watenda dhambi wasiotii katika mji huo.

**Mathayo 23:37-39 (Biblia Takatifu)**

**“Ee Yerusalemu, Yerusalemu, mji unaowaua manabii na kuwapiga mawe wajumbe wa Mungu! Ni mara ngapi nimetaka kukusanya watoto wako pamoja kama kuku hulinda vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hukuniruhusu. 38 Sasa tazama, umeachwa nyumba yako, tupu, ukiwa. 39 Kwa maana nakuambia hivi, hutaniona tena hata utakaposema, ‘Mbariki yeye ajaye kwa jina la Bwana!’”**

## 2. Mungu huchukia dhambi

Mungu anachukia dhambi, na anapenda utiifu. Mungu hachukii wenye dhambi, anawapenda. Lakini upendo Wake kwa watu wote hauimaanishi kwamba Yeye atapuuza uasi wa dhambi. Ikiwa unataka kuwa Mkristo aliyekomaa, mwenye nguvu, basi itabidi ujifunze kuwa na mtazamo sawa juu ya dhambi ambayo Mungu anao.

Wakristo wapya wanahitaji kubadilisha njia yao ya kufikiria juu ya matendo yao ya zamani ya dhambi. Nyingi ya shughuli hizi za dhambi za zamani zilikuwa majaribio ya kupata furaha katika maisha yao ya kila siku. Bado kunaweza kuwa na mvuto mkubwa wa kurudi kwenye shughuli hizo.

Njia moja ya nguvu ya kupambana na vishawishi hivyo ni kukuza mtindo mpya wa kufikiria utakaotumika wakati majaribu yanakuja. Badala ya kukubali mvuto wa jaribu, tunahitaji kuchukua msimamo na kusema, “Hapana, sitapitia tena njia hiyo. Nachagua kumtii Mungu, na kulipa kisogo jaribu hilo. Ninataka kuona jaribu hili kwa njia ile ile ambayo Mungu huchukua — Yeye huchukia dhambi, na hiyo ndiyo majibu yangu pia.”

Mabadiliko haya ya mtazamo yanaweza kuchukua muda, lakini kadiri unavyochagua jibu hili, ndivyo itakavyokuwa rahisi zaidi kupinga jaribu.

Ikiwa Mfalme Daudi alikuwa ametumia mkakati huu usiku alipomwona Bathsheba, ingemkinga kutokana na dhambi ile. Angeweza kusema moyoni mwake, “Sasa kwa kuwa ninajua mwanamke huyu ameolewa na mwanamume mwingine, sitafuata uhusiano naye. Najua Mungu anachukia uzinzi, na ninataka kuwa na mtazamo ule ule ambao Mungu anao juu ya uzinzi. Nitachagua kutembea kwa kutii sheria za Mungu.”

## 3. Mungu ni mvumilivu kwa wenye dhambi na wakristo wasiotii

Kwa sababu Mungu anatupenda Yeye ni mvumilivu kwetu. 1 Wakorintho 13:4 inaonyesha kuwa uvumilivu ni alama ya kwanza ya upendo. Mungu anatuonyesha uvumilivu wake kwa kutuzuia adhabu ya haki ambayo tunastahili pindi tunapotenda dhambi. Warumi 6:23 inasema, “Mshahara wa dhambi ni mauti.” Lakini mara nyingi, Mungu hadai malipo ya papo hapo ya mishahara hiyo kila tunapotenda dhambi.

**2 Petro 3:9 (Biblia Takatifu)**

**Bwana hasitii sana juu ya ahadi yake ya kurudi, kama watu wengine wanavyofikiria. Hapana, anakuwa mvumilivu kwa ajili yenu. Hataki mtu yeyote aangamie, kwa hivyo anatoa wakati zaidi kwa kila mtu kutubu.**

Mstari huu unaonyesha kuwa uvumilivu wa Mungu ni kielelezo cha upendo wake kwetu na hamu yake kwamba tufike mahali pa kutubu dhambi zetu.

## 4. Mungu ni Mungu wa haki

Mungu hutathmini kila tendo la utiifu na uasi kwa haki iliyo safi. Hawezi kuhongwa ili kupuuza dhambi fulani. Anajua ukweli wote. Yeye hafanyi makosa yoyote. Hahitaji msaada wowote kutoka kwetu kuamua ni ipi njia bora ya kumsahihisha mtu asiye mtiifu.

Hoja hiyo mara nyingi huibuliwa na wale wasio Wakristo, “Je, Mungu wa upendo anawezaje kuwapeleka watu kuzimu ambao hawajawahi kusikia Injili?” Tunaweza kuwa na imani kamili kwamba kila mtu atapata “hukumu ya haki” kutoka kwa Mungu.

## 5. Mungu ni Mungu wa rehema

Zaburi nyingi zilizoandikwa na Mfalme Daudi huzungumza juu ya huruma ya Mungu. Zaburi 106:1 na 107:l inasema kwamba rehema ya Mungu hudumu milele. Huruma ya Mungu ina ushawishi mkubwa kwa kila mtu ulimwenguni. Kwa sababu Mungu ni mwenye huruma, anasubiri kabla ya kutoa hukumu kwa kila mwenye dhambi. Anampa kila mtu fursa ya kuwa mtoto Wake.

Tunahitaji kuwa waangalifu kama Wakristo kwamba hatutumii vibaya faida ya rehema ya Mungu. Kwa sababu tu Mungu ni mwenye rehema hatupi uhuru wa kwenda kutenda dhambi wakati wowote tunataka na kisha kuja kwa Mungu kutafuta msamaha wake.

Unaposoma hadithi katika Biblia, mara nyingi utaona rehema ya Mungu ikifanya kazi. Mungu alimwambia Yona aende katika mji wa Ninawi, na kuhubiri ujumbe wa hukumu. Yona alimtii Mungu, na aliwasilisha wazi ujumbe wa Mungu.

**Yona 3:4 (Biblia Takatifu)**

**Siku ya kwanza, Yona alianza kuingia mjini. Alitangaza: “Siku arobaini zaidi na Ninawi itabadilishwa.”**

Mfalme aliposikia ujumbe wa Yona, alitoa wito kwa kila mtu kuacha njia zao mbaya na kumwita Mungu.

**Yona 3 8-9 (Biblia Takatifu)**

**“Nani anajua? Mungu bado anaweza kutubia na kwa huruma ageuke kutoka kwa hasira yake kali ili tusipotee.”**

Mungu alipoona kuwa watu wametubu, alijibu kwa rehema badala ya haki.

Ikiwa mtu anakataa kukiri dhambi yake, basi rehema ya Mungu labda haitabadilisha mitazamo yake.

## Hitimisho

Kuchagua kumtii Mungu ni chaguo bora zaidi unayoweza kufanya. Baraka za Mungu umeahidiwa kwako wakati unatii, na maonyo ya kutotii pia yamesemwa wazi.

**Wagalatia 6:7-8 (Biblia Takatifu)**

**Usipotoshwe. Kumbuka kwamba huwezi kumpuuza Mungu na ukaepuke nayo. Daima utavuna kile unachopanda! 8 Wale ambao wanaishi tu kutosheleza tamaa zao za dhambi watavuna matokeo ya kuoza na kifo. Lakini wale wanaoishi kumpendeza Roho watavuna uzima wa milele kutoka kwa Roho.**

Sisi sote hukosa ukamilifu katika kumtii Mungu, lakini tunaposhindwa, tunahitaji kurejea kwa Mungu mara moja ili atusaidie. Tunapokiri dhambi zetu, tunajifungua kwa rehema na msamaha wake.

Kadiri tunavyomtii Mungu kwa moyo wa upendo kwake, ndivyo tunavyopata baraka zake maishani mwetu. Tunaweza kukabili kila siku kwa ujasiri kwamba Mungu yuko tayari kutusaidia katika kila hali kujibu kwa utii. Ana nguvu zote tunazohitaji, na yuko tayari daima kutusaidia.